

# MWONGOZO WA WALIMU

*kwa*

Kitabu Cha Uamuzi Wa Afya

Informed Health Choices

# Maelezo ya Mchapishaji

**Kichwa:** Mwongozo wa Walimu kwa Kitabu Cha Uamuzi Wa Afya:  
Kujifunza kufikiria kwa makini kuhusu matibabu. Ni kitabu cha sayansi cha afya cha watoto wa shule ya msingi.

**Waandishi:** Matthew Oxman<sup>1</sup>, Sarah Rosenbaum<sup>1</sup>, Allen Nsangi<sup>2</sup>, Daniel Semakula<sup>2</sup>,  
Angela Morelli<sup>1</sup>, Astrid Austvoll-Dahlgren<sup>1</sup>, Andrew D. Oxman<sup>1</sup>, Nelson K. Sewankambo<sup>2</sup>,  
Margaret Kaseje<sup>3</sup>, Laetitia Nzirazinyonye<sup>4</sup>, Claire Glenton<sup>1</sup>, Simon Lewin<sup>1</sup>

Ilitafsiriwa kwa Kiswahili na Suzanne Z. Koteng' Nyamory, Steven Ochieng na pia Margaret Kaseje.

**Mchapishaji:** Taasisi ya Afya ya Umma ya Norway

**ISBN:** 978-82-8082-937-5 (978-82-8082-938-2: digital)

**Tarehe:** Mechi 2017

**Mtajo:** The Informed Health Choices Group. Mwongozo wa Walimu kwa Kitabu cha Uamuzi wa Afya: Kujifunza kufikiria kwa makini kuhusu matibabu. Ni kitabu cha sayansi cha afya cha watoto wa shule ya msingi. (Original title: Teachers' Guide for The Health Choices Book: Learning to think carefully about treatments. A health science book for primary school children. 2016.) Ilitafsiriwa kwa Kiswahili na Suzanne Z. Koteng' Nyamory, Steven Ochieng na pia Margaret Kaseje. Oslo: Taasisi ya Afya ya Umma ya Norway; 2018.

. ISBN: 978-82-8082-937-5 (978-82-8082-938-2: digital)

1 Kitengo cha Afya cha Ulimwengu, Taasisi ya Afya ya Umma ya Norway, Oslo, Norway

2 Chuo cha Sayansi ya Afya, Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala, Uganda

3 Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu ya Kisumu, Kenya

4 Shule ya Afya ya Umma, Chuo cha Matibabu na Sayansi ya Afya, Chuo Kikuu cha Rwanda, Kigali

Kitabu hiki kilichapishwa kama sehemu ya taarifa uchaguzi ya afya miradi ([www.informedhealthchoices.org](http://www.informedhealthchoices.org)), ambayo iliungwa mkono na halmashauri ya utafiti wa Norway, mradi nambari 220603/H10. Mfadhili hakuwa na jukumu katika kuandaa, kurekebisha maudhui.

Kitabu hiki ni leseni chini ya Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International license (<https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/>). Kulitumia matumizi ya siyo ya kibiashara, usambazaji na uzazi wa kitabu hiki kwa ruhusa, ikiwa chanzo inatolewa vizuri.

Maoni kuhusu jinsi ya kuboresha kitabu hiki yamekaribishwa na yatumwe kwa: [contact@informedhealthchoices.org](mailto:contact@informedhealthchoices.org).

## **Kuhusu mwongozo huu**

Watu kila mahali wanashambuliwa na madai kuhusu kinachoweza kuendeleza au kujeruhi afya zao. Ili kufanya uchaguzi wa utunzaji wa afya wenyewe ufahamu mzuri, lazima aweze kukadiria uaminifu wa madai hayo. Tumekuza Uchaguzi wenyewe Ufahamu wa Utunzaji wa Afya(IHC) ambayo ni rasilmali ya shule ya msingi kusaidia kwa haya.

Rasilmali hizi ni pamoja na mwongozo huu wa walimu, kitabu cha watoto\* na kitabu cha kufanyia mazoezi. Kitabu cha watoto ni pamoja na kitabu cha katuni, mazoezi na maagizo ya matendo ya darasani. Imeandikiwa watoto wa miaka 10 na zaidi. Rasilmali hizi ndizo za kwanza katika mfululizo wa rasilmali za kufunzia ili kuwawezesha watu kukadiria uaminifu wa madai na uchaguzi mzuri wa utunzaji wa afya.

Tumekuza rasilmali hizi kutoka mwaka wa 2014 hadi 2016 kupitia njia ya mpango wa msimamo wa kiutu. Hii inawahuisha watumizi wanaolengwa katika maendelezo ya mpango ka waumbaji-wenza katika vipindi vingi vya sampuli za awali, upimaji kwa watumizi na miradi ya majaribio. Tulifanya majaribio ya asili yao nchini Uganda, Kenya, Rwanda na Norway. Habari kutoka kwa watumizi yaonyesha kuwa watoto na walimu wanachukulia rasilmali hizi kuwa za faida.

Tunakadiria upeo ambao tafsiri hii ya rasilmali inavyokuza uwezo wa watoto kukadiria madai ya matibabu. Ili kulinganisha bila mapendeleo, tutazigawia nusu ya kupita shule 100 nchini Uganda hizi rasilmali za kufunzia bila utaratibu wowote. Tutapima uwezo wa watoto kukadiria madai kuhusu matibabu wakishamaliza masomo yote tisa katika Kitabu cha Uamuzi wa Afya. Halafu, tutalinganisha majibu yao na ya watoto walio kwenye shule ambazo hazipati rasilmali hizi.

Habari zaidi kuhusu rasilmali hizi na huu mradi waweza kupatikana kwenye mtandao: [www.informedhealthchoices.org](http://www.informedhealthchoices.org).

Habari kutoka kwa mtumizi kuonyesha vile rasilmali hizi zinavyoweza kukuzwa zinakaribishwa na zinaweza kutumwa kwa: [contact@informedhealthchoices.org](mailto:contact@informedhealthchoices.org).

\*Kikundi cha Ufahamu wa Uchaguzi wa Utunzaji wa Afya. Kitabu cha Uamuzi wa Afya: Kujifunza kufikiria kwa makini unapofanya uchaguzi kuhusu matibabu. Kitabu cha sayansi cha afya. Oslo: Taasisi ya Afya ya Ummaya Norway; 2016.

# **YALIYOMO**

Ukurasa

6           UTANGULIZI

16           SOMO LA 1

Afyा, matibabu na madhara ya matibabu

20           SOMO LA 2

Madai kulingana na msingi na matokeo ya kibinafsi kwa kutumia tiba

30           SOMO LA 3

Misingi mingine mibaya na madai kuhusu matibabu (Sehemu 1)

39           SOMO LA 4

Misingi mingine mibaya na madai kuhusu matibabu (Sehemu 2)

48           SOMO LA 5

Kulinganisha matibabu

56           SOMO LA 6

Kulinganisha haki ya matibabu

65           SOMO LA 7

Kulinganisha haki na watu wengi

74           SOMO LA 8

Faida na hasara za matibabu

81           SOMO LA 9

Nini cha muhimu kukumbuka kutoka kitabu hiki

88           SHEREHE

## **M pangowa muhula**

**Kabla mwanzo wa muhula,**

**Tunapendekeza kuwa uchukue asubuhi au mchana moja ili ufanye yafuatayo:**

- Jaza tarehe kwenye mpango huu
- Soma kitabu cha watoto
- Soma utangulizi wa mwongozo huu

<b>Somo</b>	<b>Ukurasa katika mwongozo</b>	<b>Matayarisho</b>	<b>Mafunzo</b>
1	Ukurasa 16	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
2	Ukurasa 20	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
3	Ukurasa 30	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
4	Ukurasa 39	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
5	Ukurasa 48	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
6	Ukurasa 56	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
7	Ukurasa 65	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
8	Ukurasa 74	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
9	Ukurasa 81	Dakika 20 Tarehe:.....	Dakika 80 Tarehe:.....
10 (Mtihani)		Dakika 15 Tarehe:.....	Dakika 90 Tarehe:.....

# **Utangulizi**

<b>Mradi huu unahusu nini na kwa nini ni muhimu?</b>	Ukurasa 6
<b>Kwa nini ni muhimu kwa watoto?</b>	Ukurasa 7
<b>Nani alitengeneza hivi vifaa na viliendelezwaje?</b>	Ukurasa 8
<b>Ni vifaa gani?</b>	Ukurasa 8
<b>Vifaa vyenyewe vinatumiwajekwa ubora zaidi?</b>	Ukurasa 12

---

## **1. Mradi huu unahusu nini na kwa nini ni muhimu?**

Mradi huu unasaidia watu kufanya uamuzi bora zaidi kwa afya yao kwa kufikiria kwa makini kuhusu matibabu. Mpe mtu samaki na watakuwa na samaki kwa siku hiyo. Mfunze huyo mtu kuvua samakina atakuwa na samaki maisha yake yote. Huu ni msemo unaojulikana vizuri sana. Cha maana ni afadhali kumfunza mtu kufanya kitu mwenyewe kuliko kuwafanyia tu.

Kuna miradi mingi inayowaeleza watu uchaguzi wa kufanya kuhusu matibabu. Miradi hii huwapa watu majibu. Mradi wa Uchaguzi wa Ufahamu wa Utunzaji wa Afya (IHC) unahusu vile mtu ye yeyote anaweza kujifanyia uchaguzi mwenyewe kwa kufikiria kwa makini. Kufikiria kwa makini kuhusu matibabu inahitaji kuuliza maswali. Kiini cha mradi huu ni maswali gani yanayofaa kuulizwa na kwa nini ya ulizwe.

Mara nyingi watu wakitaja “matibabu”, huwa wana maana ya kumeza dawa. Hata hivyo, katika mradi huu, “matibabu” ni chochote ufanyakacho ili afya yako ibaki nzuri au izidi kuwa bora. Kwa hivyo, kumeza dawa, kupasuliwa, kutumia vifaa vya tiba, kufanya mazoezi, kula au kunywa kitu, na kuepukana na kitu yote ni matibabu.

Kuna aina tatu ya maswali unayofaa kuuliza kuhusu matibabu:

- Maswali kuhusu madai ya matibabu
- Maswali kuhusu kulinganisha matibabu
- Maswali kuhusu uchaguzi wa utunzaji wa afya

### **Maswali kuhusu madai ya matibabu**

Kila mtu ana maswali kuhusu athari za matibabu. Husikika kila siku na kila pahali. Mengi ya madai haya ni ya uongo. Kwa mfano, watu walikuwa wakisema kuwa kuvuta sigara haina matokeo mabaya kwa afya yako. Hata walisema kuwa ina matokeo mazuri kwa afya yako! Hata madaktari wengine na watafiti wa afya walisema hivi!

Mara nyingi, watu hufanya uchaguzi mbaya kuhusu matibabukwa kuwa wamepotoshwa na madai mabaya kuhusu athari za matibabu hayo. Kwa mfano, watu wengi walipotoshwa kuhusu athari za sigara na wakachagua kuzivuta. Kwa kuuliza maswali kuhusu madai hayo, twavezakuzuia upotofu kwa madai yasiyoaminika ili tuweze kufanya uchaguzi unaofaa.

### **Maswali kuhusu kulinganisha matibabu**

Matibabu mengi yana matokeo mazuri na mabaya. Matibabu mengine yana matokeo tuliyo na hakika nayo. Kwa mfano, tuna uhakika kwamba kulala ndani ya neti ya kuzuia mbu, ambazo zimenyunyiziwa kiuwa dudu itazuia watu kushikwa na malaria. Hatuna hakika sana na matokeo ya matibabu mengine. Kwa mfano hatuwezi kuwa na uhakika kuhusu matokeo ya madawa mengine mapya, kwa sababu watafiti wa afya hawajayachunguza kwa makini.

Yanayopatwa na watafiti wa afya wanapochunguza matibabu yanaweza kutusaidia kufanya uchaguzi bora. Watafiti wa afya wanafaa kufanya uchunguzi wa matibabukwa makini kwa kuyalinganisha na matibabu mengine au kwa kulinganisha na kutotumia matibabu hayo. Wanafaa kupeana matibabu hayo kwa kikundi kikubwa cha watu na kupeana matibabu mengine au wasipeane matibabu kwa kikundi chengine kikubwa. Kisha walinganishe kinachowatendekea watu wa kila kikundi.

Watu wa kila kikundi wanafaa kufanana na walio katika vikundi vingine. Kama sivyo, matokeo ya watafiti wa afya yanawezakuwa ya utofauti ulioko kati ya watu bali si utofauti unaotokana na hayo matibabu. Kama si hivyo, ulinganishaji huo unaweza kutokuwa wa haki. Usipokuwa wa haki, unaweza kutupotosha. Kwa kuuliza maswali kuhusu ulinganishi wa watafiti wa afya, tunaweza kuzuia kupotoshwa na ulinganishi usio wa haki na tunaweza kufanya uchaguzi bora.

### **Maswali kuhusu uchaguzi wa utunzaji wa afya**

Unapochagua kama utumie matibabu Fulani, inakubidi ufikirie kwa makini yaliyo muhimu kwako. Matibabu mengi yana matokeo mazuri na mabaya, hata manufaa na athari. Kwa mfano, kuna matibabu ya gharama ndogo au yasiyo na gharama ambayo ni manufaa. Matibabu mengine yanagharimu pesa nyingi ambayo ni athari. Kilicho na manufaa kwako si lazima kimfaidi mtu mwengine. Kwa kuuliza maswali kuhusu uchaguzi wa utunzaji afya, unaweza kuchagua inavyokufaa mwenyewe.

---

## **2. Kwa nini haya ni muhimu kwa watoto?**

Wazazi, madaktari na watu wazima wengine huwachagulia watoto matibabu sana. Kwa mfano, watoto hawawezi na hawafai kuchagua kama wangepasuliwa. Hata hivyo, watoto pia hufanya uchaguzi wa matibabu. Kwa mfano, hao huchagua wanachokula na kunywa na wanavyofanya mazoezi. Na watoto, kama vile watu wazima, wanaweza kupotoshwa na madai ya uwongo ya matibabu.

Kufunza watoto kufanya uchaguzi mzuri ndiyo kiini cha elimu hasa elimi ya afya. Watoto watakua na mwishowe watajichagulia utunzaji wao wa afya. Ni muhimu kwao kutayarishwa kufanya huo uchaguzi. Sisi, tunaofanya kazi katika mradi huu,na wengine tumepata kuwa atoto wadogo wa hata miaka 10 wanaweza kuanza kujifunza vile wanaweza kuuliza na kujibu maswali kuhusu madai, ulinganisho na uchaguzi.

Kile watoto wanaweza kujifunza kutokana na rasilmali hizi ni ya msingi kwa sayansi yote, siyo sayansi ya afya tu. Ni muhimu kwa kufanya uchaguzi wa aina tofauti, si kwa uchaguzi kuhusu matibabu tu. Kujifunza kutokana na mtazamo wa afya unatumia mapendeleo ya asili kwa afya yake. Watu wa marika tofauti wana shauku kuu ya kujifunza vile wanaweza kutunza afya zao. Tumepata kuwa watoto pia wanapendelea kujifunza kuhusu vile twaweza kujua kinachofaa na kisichofaa kwa afya zetu.

Watu wazima wanafaa wawaaulize madaktari na wataalamu wengine wa afya mashauri kuhusu uchaguzi wa matibabu. Hata hivyo, unapopewa ushauri na mtaalamu wa afya, huwa vizuri kuuliza maswali juu ya hayo matibabu, hata ukiwa mtoto au mtu mzima. Kufanya hivi kutakusaidia wewe na huyo mtaalamu kufanya uchaguzi bora zaidi kwako.

---

### **3. Nani alitengeneza hivi vifaa na viliendelezwaje?**

Sisi, tuliotengeneza hivi vifaa, ni watafiti wa afya na wapangaji walio Uganda, Kenya, Rwanda, Norway na Uingereza. Mwanzoni mwa mradi, tulikutana na walimu tofauti nchini Uganda. Walimu walitushauri vile tunaweza kuwafunza watoto masomo yaliyoelezwa kwa muhtasari katika vifaa hivi vizuri kabisa. Tulikuwa na mawazo mengi ambayo tuliyafanyia majaribio kwa watoto na walimu wa Uganda na Norway. Tulipoamua kutengeneza kitabu na mwongozo, tulitoa toleo la kwanza la vifaa vya masomo mawili tu. Tukatoa matoleo mawili makamilifu.

Tulipima kila toleo kwa njia mbili. Kwanza, tulipeana vifaa kwa madarasa tukachunguza vile walimu na watoto walivyoziutumia. Ya pili, tuliwahoji watoto na walimu kuhusu maono yao katika matumizi ya vifaa. Tulifanya vipimo hivi nchini Uganda, Kenya, Rwanda na Norway na makumi ya walimu na mamia ya watoto. Tulitumia tulichopata katika vipimo hivi kuboresha vifaa vyenyewe. Toleo la vifaa unavyotumia ni toleo kamilifu la tatu.

---

### **4. Ni vifaa gani?**

Hivi ndivyo vifaa vya shule vya Ufahamu wa Uchaguzi wa Utunzaji wa Afya:

---

- **Mwongozo wa mwalimu**
-

Ni mwongozo wa masomo yote,kwa walimu

- **Kitabu cha watoto**

Kitabu cha kiada kilicho na hadithi na maagizo ya matendo ya kufanywa na watoto

- **Vitabu vya watoto vya mazoezi**

Kitabu cha mazoezi, cha watoto

- **Kadi za matendo**

Ni kadi za matendo ya Somo la 7, kwa walimu

- **Mabango ya makumbusho**

Mabango ya kuning'iniza darasani

- **Vifaa vingine**

-Mtihani,wa watoto

-Fomu za kutathmini masomo ya kila somo,ya walimu

## **Mwongozo wa walimu**

Huu mwongozo ni wa kukusaidia kufunza masomo tisa. Katika somo la 10, watoto watafanya mtihani. Katika mwongozo huu,kwa kila somo,kuna sehemu zilizorudiwa zitakazokusaidia kutayarisha na kufunza somo hilo:

- Malengo
- Matayarisho
- Somo

-Hatua 1: Pitia somo liliopita

-Hatua 2: Soma kwa sauti

-Hatua 3: Jadili

-Hatua 4: Ongoza tendo

-Hatua 5: Simamia mazoezi

-Hatua 6: Jaza fomu za kutathmini somo

- Usuli wa somo kwa walimu

Kurasa zote za kitabu cha watoto kiko katika mwongozo. Yamaanisha kuwa, unaweza kuona kila kitu ambacho wanaweza kuona na zaidi yake. Mwongozo na kitabu zina namba tofauti za kurasa. Kila rejeo la ukurasa katika mwongozo ina namba ya mwongozo la inapoeleza tofauti. Namba ya ukurasa wa mwongozo huwa chini ya ukurasa kwa maandishi madogo. Chini ya kurasa zingine za kitabu cha watoto,kuna maandishi yanayokuhusu ikiwa yameandikwa kwa rangi nyekundu. Haya yanatumiwa unaposoma kurasa zenyewe na darasa lako. Tumeweka tu maandishi hayo palipo na umuhimu unaofaa. Kwa kurasa nyingi,hiyo nafasi chini ya ukurasa hauna maandishi yoyote na unaweza kuitumia kuandikia maandishi yako.

Nyuma ya huu mwongozo, kuna sherehe. Sherehe ina ufanuzi wa maneno yasiyo kwenye hadithi,kwa mfano ufanuzi wa "potosha". Katika kitabu cha watoto,ufafanuzi wa maneno umerahisishwa,ili watoto waelewe kwa urahisi. Kwenye mwongozo,sherehe

inajumuisha huo ufanuzi uliorahisishwa ya watoto mbali na ufanuzi kwa ufasha ya walimu. Tumejaribu kupekana na kutumia maneno yasiyojulikana inavyoekana katika kitabu cha watoto. Kwa mfano hatutumii neno "utunzaji wa afya" hata ingawa iko kwenye kichwa cha mradi. Hata hivyo neno hilo limo katika sherehe zote.

Zingatia kwamba maneno mengine yana maana tofauti katika utafiti wa kiafya mbali na maana ambayo hujitokeleza watu wanapoyatumia. Kwa mfano, katika utafiti wa afya, "uchunguzi" unamaanisha kuzingatia kitu kwa undani zaidi kupata maelezo ya ziada juu yake, kwa mfano katika matibabu. Mara nyingi, nje ya utafiti wa afya, watu wanapotumia "uchunguzi", wana maana ya kujitayarishia kufanya kitu, kwa mfano, mtihani.

## **Kitabu cha watoto**

Vitabu vya watoto vinatarajiwa kutumiwa mara kwa mara kwa hivyo watoto wasiandikie humo.

***Hadithiyenyewe:*** Katika kitabu cha watoto, sehemu yake kuu imechukuliwa na hadithi. Inawaonyesha watoto vile malengo ya somo inavyoingiliana na maisha yao. Inakifanya kitabu kusimua na kutosahaulika. Kitabu nichenyе hadithi za katuni. Michoro inatarajiwa kuvutia na kufanya hadithi rahisi kusoma kwa watoto wanaopambana na Kiingereza au kusoma.

Hadithi yaanza katika somo la 2 na kuishia somo 8. Imegawiwa na aina tatu ya maswali kuhusu matibabu:

- Katika masomo 2, 3 na 4, hadithi inashughulikia maswali kuhusu madai ya matibabu.
- Katika masomo 5, 6 na 7, hadithi inashughulikia maswali kuhusu ulinganishi wa matibabu.
- Katika somo la 8, hadithi inashughulikia maswali kuhusu uchaguzi wa matibabu.
- Somo la 1 ni utangulizi wa kitabu. Somo la 9 ni muhtasari wa kilicho muhimu kukumbuka kutoka kitabuni.

Somo la 1 ndilo rahisi zaidi. Inafaa kuwa rahisi ili watoto wote waelewe kwa ujumla kinachoelezwa katika somo na kwa nini ni muhimu. Masomo yanazidi kuwa na changamoto. Masom 5, 6 na 7 ndiyo yenye changamoto zaidi. Yanaeleza yanayofanywa na watafiti wa afya, ambayo hayajulikani na watoto wengi. Hata hivyo, kutokana na kuendeleza vifaa hivi, tunajua kuwa watoto wanaweza kujifunza wanayopaswa kufunzwa kutoka kwenye masomo haya.

Mifano mongine humu kitabuni si halisi. Mmojawapo wa mifani hiyo iko katika somo la 6 na 7, pale ambapo wahusika katika hadithi wanajaribu kuthibitisha kama kunywa sharubeti kabla kukimbia kunasababisha uchungu mwingu zaidi tumboni kuliko kunywa maji. Wanapata kuwa kunywa sharubeti kabla kukimbia husababisha uchungu mwingu zaidi. Haya yanaweza kuwa kweli lakini watafiti wa afya hawajafanya ulinganiso wa haki kuthibitisha haya. Tumetumia mfano huu rahisi kulifanya somo lieleweke kwa watoto.

**Wahusika:** Hadithi inawahusu watoto wawili wanaoitwa Yohana na Julia. Ni ndugu. Wanakutana na profesa wawili wanaoitwa Profesa Connie Linganisha na Profesa Francis Usawa. Hawa profesa ni watafiti wa afya. Majina yao ya Linganisha na Haki ni ya kuwafanya watoto wanaosoma kitabu waweeeeze kukumbuka kile watafiti wa afya lazima wafanye ili kuwe na uhakika na matokeo ya matibabu: kulinganisha matibabu na kufanya hivyo kwa njia ya haki.

Kasuku ,ambaye ni ndege, pia ni mhusika anayetokezea mara kwa mara. Yeye ywawakilisha vile watu hawafai kufikiria kuhusu matibabu.Yeye ywarudia tu kile watu husema bila kuuliza maswali. Yeye pia ywafaa kuwafanya watoto wasisimuliwe na hadithi. Hafai kuwa na uhalisi.

**Mfuatano wa hadithi:**hadithi inaanza nyumbani kwa akina Yohana na Julia. Kidole cha Yohana kinaungua. Anachagua kupaka mavi ya ng'ombe palipoungua kutokana na kile ambacho Julia na Kasuku waliskia kutoka kwa Sara aliye rafikiye Julia. Kidole chake kinaambukizwa na Mama wawatuma Yohana na Julia kliniki. Huko kliniki,wanakutana na Profesa Usawa na Profesa Linganisha wanaowaelezea tatizo linalotokana na yaliyosemwa na Sara. Hao Profesa wanakubaliana kuwafunza Yohana na Julia masomo muhimu,ambayo wanafanya katika wiki zinazofuata. Wanakutana pahali tofauti,wanatoa mifano tofauti na kupata usaidizi kutoka watu tofauti. Mwishoni mwa hadithi, katika somo la 8, Yohana na Julia wanapata uambukizo wa masikio. Wanatumia walichojifunza kujifanyia uchaguzi ufaao.

**Maswali na mifano:** Kwa masomo mengine, kuna pia maswali ya mjadala kuhusu hadithi,mifano ya ziada ndani ya hadithi na mifano mingine baada ya hadithi.

**Matendo ya kufanywa:** Haya matendo yanafaa kuwahisisha watoto wote. Yanafaa kufafanua na kuimarisha kile watoto wanajifunza kutoka hadithini katika kila somo. Matendo haya ni rahisi na yanaweza kufanywa na madarasa ya watoto hadi 100.

**Mazoezi:** Mazoezi haya pia yanafaa kufafanua na kuimarisha kile watoto wanajifunza kutoka hadithini katika kila somo. Yanaweza kukusaidia, wewe mwalimu,kueleza aina ya usaidizi unaotakikana na uzito wa usaidizi wenyewe kwa kila mtoto.

**Orodha ya Ukumbusho:** Katika somo la 9, kuna orodha ya yaliyo muhimu kukumbuka kutoka kitabuni. Orodha hii pia inajumuishwa nyuma ya kitabu cha mazoezi.

### **Kitabu cha mazoezi cha wanafunzi**

Kuna kitabu cha mazoezi kilicho na mazoezi ya kila somo,ambayo kila mtoto anakamilisha peke yake.

### **Vifaa vingine**

Katika somo la 10,kuna mtihani. Mtihani huu ni wa kugundua kama watoto wanajifunza kutokana na kutumia vifaa hivi,pia unaweza kutumiwa kusahihisha. Kwa kila Somo,kuna fomu ya utathmini unaopaswa kujaza. Mwishowe, katika Somo la 7,kuna kundi la kadi mbili za matendo.

---

## **5. Vifaa vyenyewe vinatumiwaje kwa ubora zaidi?**

### **Mapendekezo**

Kutokana na majaribio ya rasilmali,tuna mapendekezo kadha vile unaweza kuhifadhi wakati, iwasaidie watoto kufanikisha kutimiza malengo yao na kufanya masomo kukusisimua wewe na watoto.

### **Tenga wakati wa kuyatayarisha masomo**

Nyakati zilizopendekezwa ziko katika mpango wa muhula ulioko katikaukurasa wa 7.

### **Wakubalie watoto kusoma vitabu kwa wakati wao**

Hii ni mbali na kusoma pamoja darasani wakati wa masomo.

### **Jihadhari na kuchukua wakati mwingi katika mfano mmoja**

Kunamifanomingikitabuniambayowatoto wangependa kuyajua zaidi. Hata hivyo, siyo mifano ambayo ni ya muhimu. Kilicho muhimu ni kinachoelezwa kuitumia mifano yenye. Kwa mfano, katika somo la 2, mfano uliomo kwanye hadithi ni dai kuwa mavi ya ng'ombe hutibu palipoungua. Kutokuwa ukweli siko cha umuhimu mno. Kwamba madai ya aina hiyo hayaaminiki ndicho cha muhimu kuliko yote.

### **Wahimize watoto waweze kuwa na fikira zao wenye**

Mara nyingi shulen, watoto huambiwa kukariri majibu sahihi. Kwa mfano, katika historia, huambiwa kukariri mwaka ambaa jambo lilitendeka. Katika haya masomo, watoto wanatakikana kujifunza maswali wanaofaa kuuliza ili wajitafutie kama dai linaaminika. Pia, mara nyingi shulen, watoto hufunzwa yali ambaa watu wengine hufanya. Katika masomo haya, ni muhimu kwa watoto kufikiria kile wao wenye wamefanya na watakachofanya.

### **Tambua wakati wewe au mtoto anapotoa dai kuhusu athari ya matibabu yoyote**

Kila mtu hutoa madai yasiyoaminika kuhusu athari za matibabu. Watoto na watu wazima huyafanya haya,pamoja na walimu,wazazi,madaktari watafiti wa afya na sisi, watu ambaa tulitengeneza hivi vifaa. Ni muhimu kwako,unapofunza haya masomo, kutambua wakati ambapo wewe au mtoto anatoa dai kuhusu athari ya matibabu yoyote.

Ni muhimu kwako kuhakikisha kuwa watoto wanatambua haya. Hii ni kwamba watoto watambue kuwa wafunzwayo yana umuhimu katika maisha yao ya kila siku na kuwa wanafaa kuanza kutumia wanachojifunza. Ni bora kuwa na uhakika na athari za matibabu kama tunataka kuchagua kama tutaitumia. La kusikitisha ni kuwa,mara nyingi, hatuna hakika kitakachofanyika. Hata hivyo, ni muhimu kujua uhakika unaoweza kuwa nao. Kwa maneno mengine,ni afadhali ujue kuwa huwezi kuwa na uhakika kuhusu athari zake,kuliko kufikiria kuwa unaweza kuwa na uhakika kama ki kweli. Kwa mfano,kama unachagua ikiwa unaafaa kupasuliwa,ni muhimu kuwa na uhakika kuhusu matokeo ya upasuaji. Kama umepotoshwa kufikiria kuwa unaweza kuwa na uhakikaupasuaji utakuwa salama,inaweza kukuongoza kwa uchaguzi mbaya. Hivyo

pia, ukiwa umepotoshwa kufikiria kuwa huo upasuaji ni wa kukuhatarishia maisha, inaweza kukuongoza kwa uchaguzi mbaya.

Kama unajua kuwa huwezi kuwa na uhakika kuhusu athari za upasuaji, kwa njia moja au nyingine, unaweza angaa kujiulizavile matokeo mazuri na mabaya yanavyoweza kukuathiri. Hautapotoshwa na utakuwa umejitayarisha kwa yatakayotokea.

### **Uchaguzi na urekebishaji**

Kila mwalimu na kila darasa ni tofauti. Kuna njia tofauti za kusoma, kutenda matendo na mazoezi yanayotakikana na haya masomo. Chagua njia inayokufaa zaidi na darasa lako. Hata hivyo, hakikisha kuwa unasisitiza mifano iliyoko kwenye vifaa na kumaliza hatua zote za masomo.

#### ***Kusoma***

Mnaposoma hivyo vitabu kama darasa, kuwa na uhuru wa kusimamisha maendelezo ya masomo ukifikiria kuna haja ya kueleza kitu, kwa mfano neno. Saa zingine, inasaidia kutafsiri kitu kilicho kitabuni.

Kuna njia nyingi za kusoma darasani, pamoja na:

- Kwa kila mhusika, mtoto mmoja anasoma asemacho (kutumia nafasi ya mhusika maalum)
- Mtoto mmoja, kwa nafasi iliyotengwa, awasomee wenzake darasani
- Darasa lote lissome kwa pamoja
- Ulisomee darasa

Unaweza pia kubadilisha kati ya njia hizi.

Katika mwongozo huu, kuna maagizo machache kuhusu matumizi ya ubao wa kuandikia, bali hiyo haimaanishi kwamba usiutumie. Kwa mfano, unaweza kuandika maneno muhimu ubaoni.

#### ***Mazoezi na matendo***

Ukipendelea, watoto darasani wanaweza kufanya mazoezi kabla ya matendo, kumalizia mazoezi kama kazi ya ziada nyumbani au kuyafanya pamoja katika vikundi.

Kuna njia tofauti za kusahihisha mazoezi yenye:

- Unaweza kusahihisha majibu wakati wa somo
- Usahihishe majibu baada ya somo
- Unaandika majibu sahihi ubaoni na watoto wanasahihisha majibu yao
- Unaandika majibu sahihi ubaoni na watoto wanabadilishana vitabu na kusahihishiana majibu
- Unapeana majibu sahihi kwa kikundi cha watoto wanaosahihisha vitabu vyote
- Hakikisha kuwa unawaelezea watoto majibu sahihi

# SOMO 1

## Afyा, matibabu na madhara ya matibabu

Kila kitu unachohitaji kutayarisha na kufunza hili somo:

<b>Malengo</b>	Ukurasa 15
<b>Matayarisho</b>	Ukurasa 15
<b>Somo:</b>	
Hatua 1: Pitia somo lililopita	Ukurasa 18
Hatua 2: Soma kwa sauti	Ukurasa 18
Hatua 3: Jadili	Ukurasa 18
Hatua 4: Ongoza tendo	Ukurasa 18
Hatua 5: Simamia mazoezi	Ukurasa 19
Hatua 6: Jaza fomu ya kutathmini somo	Ukurasa 19
<b>Usuli wa somo kwa walimu</b>	Ukurasa 19

---

## Malengo ya Somo la 1

Ambayo watoto wanafaa kufunzwa katika somo hili:

- "Afya" ni nini?
  - Matibabu ni nini?
  - Ni nini?"madhara ya matibabu?"
  - Ni nani "Mtafiti wa Afya?"
  - Kitabu hiki kinahusu nini?
- 

## Matayarisho ya Somo la 1(Dakika 20)

Haya ndiyo unafaa kufanya kabla ya somo.

### ***Soma mbele***

- Soma kurasa zas hili somo katika kitabu cha watoto
- Soma kurasa za somo hili katika mwongozo

### ***Kusanya vifaa***

Hakikisha uko na:

- Mwongozo huu
- Fomu ya kutathmini somo
- Vifutio

### ***Hakikisha kila mtoto ana:***

- Nakala ya kitabu cha watoto
- Vitabu vyao vya mazoezi
- Penseli au kalamu

## Somo la 1(Dakika 80)

Huu ni mpango uliopendekezwa kwa kufunza somo.

Walimu	Watoto	Wakati
<b>HATUA 1</b>	<b>Soma kwa sauti</b>	Dak 35
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza kusoma kwa sauti kutoka kitabu cha watoto. <i>Kwa njia tofauti za kusoma kwa sauti aangalia ukurasa katika mwongozo huu</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasawa 4 katika vitabu vyao na kusoma kwa sauti kulingana na maagizo.</li> </ul>	
	<i>Pumziko</i>	Dak 5
<b>HATUA 2</b>	<b>Jadili</b>	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Jadili hadithi kwa kuuliza maswali yaliyomo ukurasa unaofuatia katika mwongozo huu.</li> <li>Ikibidi, peana mifano ya ziada inayopatikana katika kurasa zinazofuata katika mwongozo huu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 3</b>	<b>Ongoza tendo</b>	Dak 15
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza tendo. Angalia kurasa zinazofuata katika mwongozo huu na ukurasa 22 wa kitabu cha watoto.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 22 katika vitabu vyao na kufanya matendo kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 4</b>	<b>Simamia mazoezi</b>	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Simamia mazoezi. Wasaidie wanafunzi wanapomaliza mazoezi yao na uongoze kusahihisha mazoezi yao. <i>Kwa njia tofauti za kusahihisha angalia ukurasa katika mwongozo huu.</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa 6 katika kitabu vyao vya mazoezi na kumaliza mazoezi.</li> </ul>	
<b>HATUA 5</b>	<b>Jaza fomu ya kutathmini</b>	Dak 5

Jaza fomu ya kutathmini somo		
------------------------------	--	--

---

## **HATUA 1 – Pitia somo lilopita**

Hakuna kupertia somo lilopita kwani ni somo la kwanza.

---

## **HATUA 2 – Kusoma kwa sauti (kitabu cha watoto ukarasa 4)**

Maandiko yanaanza ukurasa wa 4 katika ukurasa wa 4 katika kitabu cha watoto.

**Mfano ukurasa 13:** Kuna madawa ambayo yana athari kwa mtoto wakati ambapo mwanamke mjamzito akiyatumi. Athari zingine hazidhihiriki hadi miaka kadha baada ya mtoto kuzaliwa.

**Maelezo ukurasa 15:** Hiyo picha ni ya matangazo halisi iliyotumiwa kuuza sigara.

---

## **HATUA 3 – Jadili**

Haya ni maswali na majibu ya kupertia yali yaliyosomwa kwa sauti ukiwa na watoto:

### **1. Kitabu hiki kinahusu nini?**

- Hiki kitabu kinahusu kufikiria kwa makini kuhusu matibabu.

### **2.Kwa nini ni muhimu kwako kujifunza kinachoelezwa katika hiki kitabu?**

- Afya yako ni muhimu.
- Kufikiria kwa makini kuhusu matibabu kwa kuuliza maswali yatakayokusaidia kufanya uchaguzi unaofaa kuhusu afya yako.

---

## **HATUA 4 – Ongoza tendo (kitabu cha watoto ukurasa 22)**

Tendo linaanza ukurasa 22wa kitabu cha watoto.

**Maagizo:** Ni muhimu kulishughulisha daeasa lote. Waambie watoto wainue mkono kutoa jibu.Hata hivyo, waulize hata watoto wasioinua mikono wajibu.

Hii ndiyo orodha ya matokeo ya matibabu kwa matumizi ya mwalimu:

Matibabu:                   **Kuogelea**

Matokeo yawezayo kutokea:     Kufa maji (tokeo BAYA)

   Kukuongeza nguvu (tokeo ZURI)

   Ngozi kukauka (tokeo BAYA)

   Uambukizwaji (tokeo BAYA)

Matibabu:                   **Kung'oa jino bovu**

Matokeo yawezayo kutokea:     Maumivu liking'olewa (tokeo BAYA)

   Maumivu kupungua likishang'olewa (tokeo ZURI)

## **HATUA 5 – Simamia mazoezi (kitabu cha mazoezi ukurasa 6)**

Kila mtoto aandike majibu katika kitabu cha mazoezi.

### **Majibu ya mazoezi ya Somo la 1:**

#### **ZOEZI 1**

1. Afya yako ni jinsi mwili wako na akili iko.
2. Matibabu ni kitu unachofanyia afya yako.
3. Matokeo ya matibabu ni kille matibabu yanawezesha kufanyika.

#### **ZOEZI 2**

1. **Kweli** Uongo
2. Kweli **Uongo**
3. **Kweli** Uongo
4. **Kweli** Uongo
5. Kweli **Uongo**

---

## **HATUA 6 – Jaza fomu ya kutathmini somo**

---

### **Usuli wa Somo la 1 kwa walimu**

Usuli wa somo hili umeshughulikiwa katika utangulizi wa mwongozo.

## SOMO 2

### **Madai kulingana na msingi na matokeo ya kibinafsi kwa kutumia tiba**

Kila kitu unachohitaji kutayarisha na kufunza hili somo:

<b>Malengo</b>	Ukurasa 21
<b>Matayarisho</b>	Ukurasa 21
<b>Somo:</b>	
Hatua 1: Pitia somo lililopita	Ukurasa 24
Hatua 2: Soma kwa sauti	Ukurasa 24
Hayua 3: Jadili	Ukurasa 24
Hatua 4: Ongoza tendo	Ukurasa 25
Hatua 5: Simamia mazoezi	Ukurasa 27
Hatua 6: Jaza fomu ya kutathmini somo	Ukurasa 28
<b>Usuli wa somo kwa walimu</b>	Ukurasa 28

---

## Malengo ya Somo 2

Kile watoto wanafaa kujifunza katika somo hili:

- "Madai" ni nini
  - "Msingi" kwa madai ni nini
  - "Uhakika kudai" ni nini
  - Kwa nini ni muhimu kuuliza msingi kwa madai kuhusu madhara ya matibabu
  - Matokeo ya mtu binafsi kutumia matibabu ni msingi mbaya kuhusu madhara ya matibabu
- 

## Matayarisho ya Somo 2(Dakika 20)

Unachofaa kufanya kabla somo hilo.

### **Soma mbele**

- Soma kurasa za somo hili katika vitabu vya watoto
- Soma kurasa za somo hili katika mwongozo

### **Kusanya vifaa**

Hakikisha una:

- Mwongozo huu
- Fomu ya kutathmini somo hili
- Vifutio

### **Hakikisha kuwa kila mtoto ana:**

- Nakala ya kitabu cha watoto
- Vitabu vyao vya mazoezi
- Penseli au kalamu

**Hadithi kwa ufupi:** Yohana na Julia wanachemsha maji nyumbani. Kasuku wanamshua Yohana, kwa hivyo anayagonga maji na kuchomwa kidole. Kasuku anasema kwa kelele, "Mavi ya ng'ombe hutibu palipoungua!" Hii inamkumbusha Julia wakati ambapo Sara alitoa dai kama hilo. Kiini cha dai la Sara ni tajriba yake mwenyewe ya kupaka mavi ya ng'ombe palipoungua na pakapona. Julia anamwambia Yohana apake mavi ya ng'ombe palipoungua na anafanya hivyo. Kufikia kesho yake, kidole cha Yohana kilikuwa kimeambukizwa. Mama anawatuma Yohana na Julia kwenda kliniki, wanapokutana na Profesa Connie Linganisha na Profesa Francis Usawa. Hao Profesa wanaeleza kwa nini tajriba ya Sara mwenyewe ilikuwa na kiini kibaya kwa dai lake.

## Somo 2 (dakika 80)

Hii ni mpango wa kufundisha somo hili lililopendekezwa.

Walimu	Watoto	Wakati
<b>HATUA 1</b>	<b>Pitia somo lililopita</b>	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Pitia somo lililopita kwa kuuliza maswali kwenye ukurasa ufuatao.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali unavyoagizwa.</li> </ul>	
<b>HATUA 2</b>	<b>Soma kwa sauti</b>	Dak 25
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza kusoma kwa sauti kutoka kitabu cha watoto. <i>Kwa njia tofauti za kusoma kwa sauti aangalia ukurasa katika mwongozo huu</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 28 katika vitabu vyao na kusoma kwa sauti kulingana na maagizo.</li> </ul>	
	<b>Pumziko</b>	Dak 5
<b>HATUA 3</b>	<b>Jadili</b>	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Jadili hadithi kwa kuuliza maswali yaliyomo ukurasa unaofuatia katika mwongozo huu.</li> <li>Ikibidi, peana mifano ya ziada inayopatikana katika kurasa zinazofuata katika mwongozo huu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 4</b>	<b>Ongoza tendo</b>	Dak 15
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza tendo. Angalia kurasa zinazofuata katika mwongozo huu na ukurasa 42 wa kitabu cha watoto.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 42 katika vitabu vyao na kufanya matendo kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 5</b>	<b>Simamia mazoezi</b>	Dak 10

<ul style="list-style-type: none"> <li>Simamia mazoezi. Wasaidie wanafunzi wanapomaliza mazoezi yao na uongoze kusahihisha mazoezi yao.</li> </ul> <p><i>Kwa njia tofauti za kusahihisha angalia ukurasa katika mwongozo huu.</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa 10 katika vitabu vyao vya mazoezi na maliza mazoezi.</li> </ul>	
<b>HATUA 6</b>	<b>Jaza fomu ya kutathmiini</b>	Dak 5
Jaza fomu ya kutathmini somo		

---

## HATUA 1 – Pitia somo lililopita

Haya ni maswali na majibu ya kupitia somo lililopita, na watoto.

### 1. Hiki kitabu kinahusu nini?

- Kitabu hiki kinahusu vile unaweza kufikiria kwa makini kuhusu matibabu.

### 2. Kwa nini ni muhimu kwako kujifunza kinachosemwa kitabuni?

- Afya yako ni muhimu.
- Kufikiria kwa makini kuhusu matibabu kwa kuuliza maswali kutakusaidia kufanya uchaguzi bora zaidi kwa afya yako.

---

## HATUA 2 – Soma kwa sauti (kitabu cha wanafunzi ukurasa 28)

Maandiko yanaanza ukurasa 28 katika kitabu cha wanafunzi.

**Maagizo:** Popote palipo na kisanduku kwenye katuni kilicho na maandishi kidogo au bila chochote, kama katika ukurasa wa 30 au 31, koma na uwaulize wanafunzi darasani mwako kueleza kinachofanyika.

**Maelezo ya ukurasa 38** "Kiini" ni kwa umoja ("kiini kimoja"). "Viini" ni kwa wingi ("viini viwili au zaidi").

**Maelezo ya ukurasa 39:** Tajriba ya mtu mwenyeweni kiini kizuri cha dai kuhusu kitu ambacho kila mara hufanyika. Kwa mfano, tajriba yako ya kujichoma kidole unaposhika sufuria moto ni kiini kizuri cha kudai kuwa kushika sufuria moto itakuchoma kidole.

---

## HATUA 3 – Jadili

Haya ndiyo maswali na majibu ya kupitia somo lililopita na watoto.

### 1. Dai la Sara ni lipi?

- Mavi ya ng'ombe hutibu palipoungua.

### 2. Kiini cha dai la Sara liliwuwa lipi?

- Tajriba yake mwenyewe ya kupaka mavi ya ng'ombe palipoungua.

### 3. Kwa nini dai lake halikuaminika?

- Kiini cha dai lake kilikuwa kibaya. Inawezekana kuwa palipoungua pangepona bila kupapakia mavi ya ng'ombe.

## Mifano ya ziada ya kuwapa watoto, ikibidi

Hii ni mifano ya ziada yanayoweza kusaidia kueleza kile ambacho watoto wangejifunza kutoka kwenye hadithi. Tumia tu mifano hii ikibidi.

*Kwa nini tajriba ya mtu mwenyewe kutumia matibabu ni kiini kibaya cha dai kuhusu matokeo ya matibabu:*

**Dai:** "Rafiki yangu anasema ati kunywa chai kunapunguza maumivu kwa sababu alikunywa chai na maumivu yake ya kichwa yakapoteal!"

**Matibabu:** Kunywa chai

**Matokeo:** Maumivu kupungua

**Kiini:** Tajriba ya rafiki mwenyewe baada ya kunywa chai

**Maelezo:** Tajriba ya rafiki yake mwenyewe ni kiini kibaya cha dai. Inawezekana kuwa kichwa chake kingepona hata kama angekunywa chai au la. Dai hili haliaminiki.

**Dai:** "Dadangu anasema kuwa kumeza dawa hii hutuliza homa kwa sababu alimeza moja ikamtilizia!"

**Matibabu:** Kumeza dawa

**Kiini:** Kutuliza homa

**Basis:** Tajriba ya dadake mwenyewe ya kumeza dawa

**Maelezo:** Tajriba hii ya dadake mwenyewe ni kiini kibaya cha dai hili. Inawezekana kuwa homa ingetulia hata angemeza dawa au la. Dai hili haliaminiki.

---

## **HATUA 4 – Ongoza tendo (kitabu cha watoto ukurasa 42)**

Tendo hili linaanza ukurasa 42 wa kitabu cha watoto.

**Maagizo ziada Hatua 1:** Hadithi iko kwenye mwongozo huu katika kurasa zilizoko baada ya mfano. Hakikisha inasomwa kwa utaratibu ila watoto wapate nafasi ya kutoshaya hatua inayofuata.

**Hatua 2:** Kama kuna dai hadithini, lakini haitambuliwi na mtoto ye yeyote, koma na ueleze kwa nini ni dai na matokeo ya matibabu.

**Hatua 3:** Waambie watoto wainue mkono kujibu kutoa majibu. Hata hivyo, waulize hata wale wasioinua mkono watoe majibu. Ni muhimu kujumuisha darasa lote.

### **Hadithi la tendo hilo**

Yohana ana uchungu kooni... Si mbaya sana lakini inamtatiza kwa kiasi anapomeza chakula... Mama amewatuma Yohana na Julia kununua tiba... Barabarani, wanaona tangazo kubwa la kinywaji kipy Cha nguvu kinachoitwa Sharubati ya Nguvu... Imeandikwa hivi kwenye kibao: "Sharubati ya Nguvu inakufanya uwe mwenye nguvu!"

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kunywa Sharubati ya nguvu na matokeo ni kukufanya uwe mwenye nguvu.*

Julia anamwambia Yohana, "Nilikunywa Sharubati ya Nguvu siku moja, bali sikupata nguvu zaidi...kwa hivyo Sharubati ya Nguvu hikuongezi nguvu!"

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kunywa Sharubati ya Nguvu na matokeo ni kukuongeza nguvu (haina matokeo).*

Hata hivyo, Julia anasema, "Ilikuwa tamu..." Yohana na Julia wakafika katika duka la kijiji chao...Mwenye duka, Bw. Semakula,yuko..."Habari za mchana Yohana na Julia," Bw. Semakula akasema... "Nzuri Bw. Semakula," Yohana na Julia... Yohana akasema kuwa alisikia kuwa kula machungwa hutibu koo chungu...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kula machungwa na matokeo ni koo chungu kupona.*

Bw. Semakula akasema kuwa hiyo si kweli...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kula machungwa na matokeo ni haitibu koo chungu (haina matokeo).*

Bw. Semakula akasema Yohana angenunua majani badala yake ...Akasema kuwa kunywa chai kungemtibu koo yake chungu...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kunywa chai na matokeo ni kutibu koo chungu.*

Yohana na Julia hawajui cha kufanya ...Wanamshukuru Bw. Semakula, lakini wanaamua kwenda kwa duka la kuuza madawa kununua dawa...Huko duka la madawa, Bi. Namutebianafanya kazi... Yohana na Julia wanamsalimia na kimuuliza dawa ambayo ingemfaa Yohana kwa koo yake...Bi. Namutebi anasema kuwa kuna madawa tofauti ambayo Yohana angetumia... "Hii dawa ya kunywa ya kukohoa itaitibu hiyo koo yako chungu,"akasema...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kunywa dawa ya kukohoa na matokeo ni kutibu koo chungu..*

Au waweza kumeza hizi tembe...Hii tembe itakutulizia maumivu ukungojea koo yako kupona...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kumeza tembe na matokeo ni kutibu maumivu ya ishe.*

Hata hivyo, Bi. Namutebi akasema kuwa, wakati mwininge, tembe hizo huleta maumivu ya tumbo...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kumeza tembe na matokeo ni kusababisha maumivu ya tumbo.*

Yohana na Julia wakanunua tembe kadha... Walipofika nyumbani, Yohana akaimeza moja... Mamaakamwambia Yohana aende akapumzike... Alisema kupumzika humfanya mtu kuhisi vizuri kila mara...

*DAI! Hili ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kupumzika na matokeo ni kuhisi vizuri.*

Yohana akalala kupumzika... Kwa ghafla, Kasuku anaonekana dirishani na kuanza kupiga kelele, "MACHUNGWA HUPONYA KOO CHUNGU!"

*DAI! Hii ni dai kuhusu matokeo ya matibabu. Matibabu ni kula machungwa na katokeo ni kutibu koo chungu.*

Mwisho.

**Kuhusu mfano wa tendo hili:** Mara nyingi, koo chungu hupona yenewe. Hata hivyo, kama mtoto ana homa kali pamoja na koo chungu au kama mtoto hataki kula au kunywa kwa sababu uchungu ni mwangi, inafaa wapelekwe kumwona daktari au muuguzi. Kama mtoto anapumua kwa shida au anashindwa kumeza, ywatokwa na mate mengi au shingo imefura au imeganda, huyo mtoto anafaa kupelekwa hospitali au kliniki. Ili kupunguza maumivu ya koo chungu zisizo mbaya sana, kama ya Yohana kwenye hadithi, kunywa chai moto, supu au kinywaji baridi inaweza kusaidia. Mtoto lazima anywe maji ya kutosha, hata kama anasikia uchungu akinywa. Kituliza maumivu (tembe za kutuliza maumivu), kama Panadol, inaweza kusaidia, lakini mtoto asipewe aspirin.

---

## HATUA 5 – Simamia mazoezi (kitabu cha mazoezi ukurasa 10)

Watoto waandike majibu katika vitabu vyao vya mazoezi.

### Majibu ya mazoezi ya Somo 2:

#### ZOEZI 1

1. Dai kitu kisemwacho na mtu ambacho kinawenza kuwa ukweli au uongo.
2. Kiini cha dai ni msingi kinachoegemea au sababu ya kutoa dai lenyewe.
3. Dai lisiloaminika ni dai lililo na kiini kibaya.
4. Tajriba ya mtu mwenyewe ya kutumia matibabu ni kitu kilichotendeka pia.

#### ZOEZI 2

1. *Tajriba ya Anderea:* Kula tufaha na meno yake yakang'oka.  
*Dai la Anderea:* Kula matufaha itafanya meno yako yatang'oka.
2. *Tajriba ya Danieli:* Kuoga kwa maji ya moto na homa yake ikakaribia kuisha baada ya saa moja.  
*Dai la Danieli:* Kuogakwamajiyamoto itatibu homa.
3. *Tajriba ya Kristina:* Kulala kwa masaa 12 na kushinda mbio.  
*Dai la Kristina's claim:* Kulala kwa muda mrefu utakufanya uwe na mbio zaidi.

#### ZOEZI 3 Maagizo ya ziada:

Waambie watoto wafungue ukurasa 46 ya vitabu vyao vya mazoezi.Waagize kujaza tu mistari mitatu ya kila dai wanalokusanya, hadi Somo la 9.

Kwa mfano:

Dai: Kunywa sharubeti hutibu mafua  
Matibabu: Kunywa sharubeti  
Matokeo: Kutibu mafua

Katika Somola 9, watajaza misingi ya madai na kuweka alama kwenye visanduku kuonyesha kama wanafikiria kuwa kila dai linaaminika au hawana uhakika. Lengo la zoezi ni ili watoto watambue kuwa wanasikia madai mengi kuhusu matokeo ya matibabu,na mengi ya madai hayo hayaaminiki.

---

## HATUA 6 – Jaza fomu ya kutathmini somo

---

### Usuli wa somo la 2 kwa walimu

“Dai” linaweza kumaanisha vitu tofauti.Katika kitabu hiki,ina maana moja tu:In this book, it only means one thing: kitu ambacho mtu anasema ambacho kinaweza kuwa sahihi au si sahihi. Kila mtu hutoa madai ya aina hii. Mara nyingi, tunapodai kitu, Hutoa dai lenyewe kama ambayo inaaminika kikamilifu. Kwa maneno mengine, tunasema kitu kama ambacho ni jambo la hakika, huku ni dai tu kwa ukweli. Madai mengi hayaaminiki,kwa hivyo ni muhimu kutambua mtu atoapo dai. Ukiamini dai lisiloaminika kuhusu matokeo ya matibabu, unafanya uchaguzi mbaya kuhusu matibabu hayo.

Kuepukana na kupotoshwa kwa madai yasiyoaminika, lazima tuijilize: Kiini cha dai lenyewe ni nini? “Kiini” yaweza kuwa na maana tofauti, lakini katika kitabu hiki kinamaanisha sababu ya mtu kusema au kufanya kitu. Kuna misingi mingi ya kudai kitu. Uaminifu wa dai unatokana na kiini chake. Watafiti wa afya mara nyingine husema “ushahidi” unaouunga mkono dai, kuliko “kiini” cha dai.

Watafiti huuliza maswali na kutafuta majibu ili kujua mengi kuhusu dunia. Kuna watafiti aina tofauti wanaofanya utafiti wa aina tofauti. Watafiti wa afya hutafuta majibu ya maswali kuhusu afya. Kuna aina tofauti ya utafiti wa afya pia, lakini kitabu hiki inahusika na aina moja: kuuliza maswali na kutafuta majibu kuhusu matokeo ya matibabu.

Tajriba ya mtu mwenyewe ndiyo mojawapo wa njia za misingi ya madai kuhusu matokeo ya matibabu inayojulikana. Aina nyingi za tajriba ya mtu mwenyewe ni muhimu na tunafaa kujifunza kitu kutoka kwao. Kwa mfano, matibabu mengi yana matokeo madogo, lakini machache yana matokeo makubwa, yanayoonekana wazi.Kwa watu wengi, kuvaan miwani ina matokeo makubwa yaliyo wazi kuhusu vile

wanavyoweza kuona vizuri. Tajriba yao ya kuva miwani imetosha kujua kwamba wanafaa kuva miwani.

Matibabu mengi hayana matokeo makubwa. Kwa hivyo, mara nyingi, tajriba ya mtu binafsi kutumia matibabu ni kiini kibaya cha dai kuhusu matokeo. Watafiti saa zingine husema “ushahidi wa hadithi za ukweli” au “kuchunguza kesi ya mtu,” kuliko “tajriba ya mtu binafsi.” “Ushahidi wa hadithi ya mtu binafsi” ni hadithi fupi kuhusu kitu cha ukweli. Hadithi hiini kiini kibaya kwa dai kuhusu matokeo ya matibabu, hata kama hadithi yenye ni ya ukweli. Kwa mfano, wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa homa ya ndege (mafua ya ndege), watu wengine walioambukizwa na homa ya ndege walipewa dawa iliyoitwa Tamiflu. Ni ukweli kuwa wengine kwa watu hao walipona. Hata hivyo, hadithi hizo za ukweli zilikuwa misingi mibaya kwa dai kuwa Tamiflu inatibu homa ya ndege. Inawezekana kuwa hao watu wangepona bila hiyo dawa.

## Somo 3

### **Misingi mingine mibaya na madai kuhusu matibabu (Sehemu 1)**

Kila kitu unachohitaji kutayarisha na kufunza hili somo:

<b>Malengo</b>	Ukurasa 31
<b>Matayarisho</b>	Ukurasa 31
<b>Somo:</b>	
Hatua 1: Pitia somo lililopita	Ukurasa 34
Hatua 2: Soma kwa sauti	Ukurasa 34
Hatua 3: Jadili	Ukurasa 34
Hatua 4: Ongoza tendo	Ukurasa 35
Hatua 5: Simamia mazoezi	Ukurasa 37
Hatua 6: Jaza fomu ya kutathmini somo	Ukurasa 37
<b>Usuli wa somo kwa walimu</b>	Ukurasa 38

---

## Malengo ya Somo 3

Kile wanafunzi wanafaa kujifunza katika somo hili:

Kwa nini hii ni misingi mbaya kwa madai kuhusu madhara ya matibabu:

1. Ni kwa muda gani matibabu yamekuwa yakitumika au watu wangapi wameyatutia
  2. Kiasi gani cha fedha inagharamia matibabu au upwa wake
- 

## Matayarisho Somo 3 (Dakika 30)

Haya ndiyo wapaswa kufanya kabla somo hili.

### ***Soma mbele***

- Soma kurasa za somo hili katika kitabu cha watoto
- Soma kurasa za somo hili katika mwongozo

### ***Kusanya vifaa***

Hakikisha una:

- Mwongozo huu
- Fomu ya kutathmini somo
- Vifutio

### ***Hakikisha kila mtu ana:***

- Nakala ya kitabu cha watoto
- Vitabu vyao vya mazoezi
- Penseli au kalamu

***Hadithi kwa ufupi:*** Profesa Linganisha na Profesa Haki walimzuru Yohana na Julia katika shule yao ya msingi. Yohana na Julia walishakusanya madai kutoka kwa marafiki zao. Hao Profesa walichagua madai hayo mawili kutumia kama mifano. Mifano hiyo ilikuwa kuelezea misingi mibaya mingine ya madai kuhusu matokeo ya matibabu. Kwanza, Profesa hao walitumia dai la Ruth kama mfano. Dai lake lilihusu madawa ya mitishamba. Ya pili, hao Profesa walitumia dai la Ahmed kama mfano. Dai lake lilihusu miwani zake mpya.

## Somo 3 (dakika 80)

This is a suggested plan for teaching the lesson.

Walimu	Watoto	Wakati
HATUA 1	Pitia somo lililopita	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Pitia somo lililopita kwa kuuliza maswali katika ukurasa ufuatao.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 2	Soma kwa sauti	Dak 25
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza kusoma kwa sauti kutoka kitabu cha watoto. <i>Kwa njia tofauti za kusoma kwa sauti aangalia ukurasa katika mwongozo huu</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 48 katika vitabu vyao na kusoma kwa sauti kulingana na maagizo.</li> </ul>	
	Pumziko	Dak 5
HATUA 3	Jadili	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Jadili hadithi kwa kuuliza maswali yaliyomo ukurasa unaofuatia katika mwongozo huu.</li> <li>Ikibidi, peana mifano ya ziada inayopatikana katika kurasa zinazofuata katika mwongozo huu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 4	Ongoza tendo	Dak 15
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza tendo. Angalia kurasa zinazofuata katika mwongozo huu na ukurasa 57 wa kitabu cha watoto.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 57 katika vitabu vyao na kufanya matendo kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 5	Simamia mazoezi	Dak 10

<ul style="list-style-type: none"> <li>Simamia mazoezi. Wasaidie wanafunzi wanapomaliza mazoezi yao na uongoze kusahihisha mazoezi yao.</li> </ul> <p><i>Kwa njia tofauti za kusahihisha angalia ukurasa katika mwongozo huu.</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa 16 katika vitabu vyao vya mazoezi na maliza mazoezi.</li> </ul>	
<b>HATUA 6</b>	<b>Jaza fomu ya kutathmiini</b>	Dak 5
Jaza fomu ya kutathmini somo		

---

## HATUA 1 – Pitia somo lililopita

These are questions and answers for reviewing the previous lesson, with the children.

### 1. Dai la Sara ni lipi?

- Mavi ya ng'ombe hutibu palipoungua.

### 2. Kiini chadai la Sara ni kipi?

- Tajriba yake mwenyewe ya kupaka mavi ya ng'ombe palipoungua.

### 3. Kwa nini dai lake halikuaminika?

- Kiini cha dai lake lilikuwa baya. Kuna uwezekano kuwa palipoungua pangepona bila kuipakia mavi ya ng'ombe.

---

## HATUA 2 – Soma kwa sauti (kitabu cha wanafunzi ukurasa 48)

Maandishi yanaanza ukurasa 48 katika kitabu cha watoto.

**Usuli wa ukurasa 53:** Watafiti wa afya waligundua kuwa mitishamba mingine ina matokeo mazuri. Kwa mfano, malai/siagi ya pilipili kali sana inapunguza maumivu ya mgongo. Hata hivyo, wamepata kuwa mitishamba mingine yana matokeo madogo au yasiyo mazuri, na mengine yana athari mbaya. Kwa mfano, kutafuna tunda la mtambuu inasababisha sarataniya mdomo. Kuna mitishamba mingi ambayo hayajachunguzwa kwa makini.

**Usuli wa ukurasa 55:** Watu wengi wanatumia miwani ili waone kwa njia bora zaidi. Wengine, bila miwani, wanang'ang'ana kuona kilicho karibu nao. Wanaona tu vya mbali vizuri. Wengine hawayaoni yaliyo mbali ipasavyo. Hawa ni wa kuona vya karibu tu. Ili miwani imsaidia mtu kuona vizuri, miwani lazima yarekebishwe kulingana na umbali unaona. Matokeo hayategemei kama miwani ni mpya au ilinunuliwa kwa gharama kubwa.

---

## HATUA 3 – Jadili

Haya ni maswali na majibu ya kuitia somo lililopita, na watoto.

### 1. Dai na Ruth ni lipi?

- Dai la Ruth lilikuwa kwamba mitishamba yake hutibu magonjwa.

### 2. Kwa nini dai la Ruth halikuaminika?

- Kiini cha dai la Ruth kilikuwa kwamba watu wengi walishatumia mitishamba kwa muda mrefu. Watu wangapi washatumia matibabu au muda ambao walitumia ni misingi mibaya kwa madai kuhusu matokeo ya matibabu. Kuna

matibabu mengi ambayo watu wemetumia kwa muda mrefu ambayo yana matokeo mengine kuliko vile watu walifikiria – kwa mfano, kupaka mavi ya ng'ombe palipoungua..

### 3. Dai la Ahmed ni lipi?

- Dai la Ahmed lilikuwa kwamba miwani yake ilikuwa bora kuliko zingine zote.

### 4. Kwa nini dai la Ahmed halikuaminika?

- Kiini cha dai la Ahmed ilikuwa kwamba miwani yake ilikuwa mpya na iligharimu pesa nyingi kuliko zingine zote. Vile matibabu yako mpya au yalivyogharimu ni viini vibaya kwa madai kuhusu matokeo. Matibabu ya zamani ambayo hayakuwa na gharama kuu yanaweza kuwa mazuri au bora zaidi kuliko matibabu mapya. Ahmed alikuwa anaona vizuri na miwani yake kama vile aonavyo na hizo mpya.

## Mifano ya ziada kuwapa wanafunzi, ikibidi

Hii ni mifano ya ziada kusaidia kueleza kile watoto wangejifunza kutoka kwa hadithi. Tumia tu mifani hii ukufikiria inabidi.

*Kwa nini muda ambao matibabu umetumiwa au watu wangapi wameyatumiани viini vibaya vya madai kuhusu matokeo ya matibabu:*

**Dai:** "Kuna mchawi katika kijiji cha kina nyanyangu anayetibu magonjwa! Najua kwa sababu watu wengi wamemwenda huyu mchawi wakiwa wagonjwa!"

**Matibabu:** Kutumia uganga

**Matokeo:** Kutibu magonjwa

**Kiini:** Idadi ya watu ambao wamemwenda mchawi wakiwa wagonjwa

**Maelezo:** Kutumia idadi ya watu ambao wamemwenda huyo mchawi ni kiini kibaya kwa hilo dai.

Kuna uwezekano kuwa uganga hauna matokeo au hauna matokeo mabaya. Dai hili haliaminiki.

*Kwa nini gharama ya matibabu au vile ni matibabu mapya ni viini vibaya kwa madai kuhusu matokeo ya matibabu:*

**Dai:** "Kirimu hii inagharimu pesa nyingi! Ukiitumia, ngozi yako itakuwa nyororo kuliko ukitumia kirimu nyingine!"

**Matibabu:** Kutumia hiyo kirimu

**Matokeo:** Kuwa na ngozi nyororo zaidi

**Kiini:** Bei yake

**Maelezo:** Bei ya kirimu ni kiini kibaya kwa dai hilo. Kuna uwezekano kuwa kirimu zingine zilizo na bei ndogo kuishinda pia ni nzuri kama hiyo au hata ni bora zaidi. Dai hilo haliaminiki.

---

## HATUA 4 – Ongoza tendo(kitabu cha watoto ukurasa 57)

Tendo linaanza ukurasa wa 57 katika kitabu cha watoto.

**Maelezo ziada:** Andika viini ambavyo watoto wameshajifunza katika ubao.

- Tajriba ya mtu binafsi anayetumia matibabu
- Muda ambao matibabu umetumiwa au idadi ya watu ambao wamiyatumia
- Bei ya matibabu au upya wake

**Hatua 12:** Waambie watoto wainue mkono kujibu maswali. Hata hivyo, waulize hata wasioinua mkono pia wajibu. Ni muhimu kulijumuisha darasa lote.

### **Orodha ya madai ya kutumiwa katika tendo**

*Dai la Rashida: "Nilipokuwa najifunza kuendesha balskeli, niliomba kofia ya kinga ya rafiki yangu. Baadaye, nikapata nina chawa! Kuvalaa kofia ya kinga inakupa chawa!"*

**Matibabu:** Kuvalaa kofia ya kinga

**Matokeo:** Kupata chawa

**Kiini:** Tajriba ya Rashida mwenyewe kuvalaa hiyo kofia ya kinga

**Maelezo:** Dai haliaminiki. Kofia za kinga nyingi hazina chawa.

*Dai la Antoni: "Hizi ndizo aina mpya ya plasta! Zinafanya vidonda vinapona haraka kuliko plasta zinazouzwa katika duka!"*

**Matibabu:** Kuvishwa mojawapo ya hizo plasta mpya

**Matokeo:** Kufanya kidonda kipone haraka

**Kiini:** Upya wa hizo plasta

**Maelezo:** Dai hilo haliaminiki. Kuna uwezekano kuwa vidonda hupona haraka kama au haraka kushinda ukivishwa plasta za zamani. Pia kuna uwezekano kuwa kuvalaa plasta mpya au za zamani hazisaidii kidonda kupona haraka.

*Dai la Olivia: "Kila mtu anajua kuwa kula karoti kunakufanya uone vizuri usiku usiku!"*

**Matibabu:** Kula karoti

**Matokeo:** Kuweza kuona vizuri zaidi usiku

**Kiini:** Idadi ya watu ambao wametumia karoti na kuwezesewa kuona vizuri zaidi usiku

**Maelezo:** Dai hilo haliaminiki. Kuna uwezekano kuwa kula karoti hauna uhusiano na unavyoona vizuri zaidi usiku.

*Dai la Rhoda: "Kila mara napatapo homa, mimi hula kitunguu thumu na napona. Watu wamefanya hivi, kwa hivyo ni matibabu mazuri!"*

**Matibabu:** Kutafuna kitunguu thumu

**Matokeo:** Kutibu homa

**Kiini:** Idadi ya wakati ambao watu wametafuna kitunguu thumu kutibu homa

**Maelezo:** Dai hili haliaminiki. Kuna uwezekano wa kutafuna kitunguu thumu na kusiwe na tofauti katika homa.

*Dai la Erik: "Hivi viatu vya kuchezza kandadnda ni bei ghali! Thamani yake yafaa kwa sababu zitaniwezesha kupiga teke kwa nguvu zaidi!"*

**Matibabu:**Kuva viatu vya kandanda

**Matokeo:** Kupiga teke kwa nguvu zaidi

**Kiini:**Thamani ya bei ya viatu vyenyewe

**Maelezo:** Dai hili haliaminiki.Kuna uwezekano wa Erik anapiga teke kwa nguvu au kwa nguvu zaidi hata akivaa viatu vyake vya zamani.

*Dai la Arnoldi: "Nilikuwa na mafua, lakini nikalala kwa saa moja mchana na baadaye mafua ikapotea !Lazima kuwe kuwa kulala mchana kunatibu mafua!"*

**Matibabu:**Kulala kwa saa moja mchana

**Matokeo:**Kutibu mafua

**Kiini:**Tajriba ya Arnoldi mwenyewe

**Maelezo:**Kuna uwezekano kuwa mafua ya Arnoldi yangeisha hata kama asingelala kwa hiyo saa moja mchana.

## HATUA 5 – Simamia mazoezi(kitabu cha mazoezi ukurasa16)

Watoto waandike majibu katika vitabu vyao vya mazoezi.

**Maagizo ya ziada:**Wakumbushe watoto kukusanya madai nyuma ya vitabu vyao.

### Majibu ya mazoezi katika Somo 3:

#### ZOEZI 1

1. Kweli **Uongo**
2. **Kweli** Uongo
3. Kweli **Uongo**
4. Kweli **Uongo**
5. **Kweli** Uongo

#### ZOEZI2

1. *Dai haliaminiki kwa sababu:*Kiini cha dai hili ni tajriba ya Michael ya kuoga kwa maji ya moto alipokuwa na homa. Kunawezekana kuwa homa ingeisha haraka hivyo hata bila yeye kuoga.
2. *Dai haliaminiki kwa sababu:*Kiini cha dai ni bei ya kahawa. Inawezekana kwamba kahawa inaweza kuwa ya manufaa kwa afya yako au hata bora zaidi, hata kama haina gharama kuu sana kama hiyo.

## HATUA 6 – Jaza fomu ya kutathmini somo

### Usuli wa Somo la 3 kwa walimu

Mara nyingi, matibabu ya kawaida na ya kidesturi yana matokeo mengine kuliko vile watu wanafikiria. Kwa mfano, mamia ya miaka iliyopita, wakati wa Miaka ya Kati, ilikuwa ni imani ya kawaida kuwa kuwatoa watu damu (kudunga ngozi zao na kuwacha damu itiririke) kungewaponya magonjwa. Leo hii, tuna hakika kuwa matibabu haya yana matokeo mengine kuliko watu walivyofikiria. Hata ingewaua watu. Kwa hivyo, idadi ya watu walotumia matibabu au muda gani ambao washautumia ni kiini kibaya cha madai kuhusu matokeo ya matibabu.

Upyawamatibabuauthamaniyabeiyakepianikiinikibayachamadaiyamatokeo.

Mara nyingi, matibabu mapya na yenye gharama ya juu kuliko mengine yana matokeo sawa au hata mabaya zaidi. Kwa mfano, madawa mengine ya kusugulia meno ni mapya na ghali kuliko mengine, lakini mengi yao yana matokeo sawa kwa vile mara nyingi. yametengenezwa kwa viambao sawa. Pia, matokeo mengine mabaya hayaonekani hadi muda mrefu baada ya matibabu. Kwa hivyo, hatuwezi kuwa na uhakika kuhusu matokeo mabaya ya matibabu mapya. Kwa mfano, kulikuwa na dawa ilijojulikana kama Vioxx iliyotumiwa kwa maumivu na mamilioni ya watu. Kampuni iliyotengeneza Vioxx iliikuza kila pahali kwa kutumia matangazo. Hata hivyo, watafiti wa afya mwishowe walipata kuwa dawa hiyo ilisababisha afkani/mshtuko wa moyo na kiharusi.

## SOMO 4

### **Misingi mingine mibaya na madai kuhusu matibabu (Sehemu 2)**

Kila kitu unachohitaji kutayarisha na kufunza hili somo:

<b>Malengo</b>	Ukurasa x
<b>Matayarisho</b>	Ukurasa x
<b>Somo:</b>	
Hatua 1: Pitia somo lililopita	Ukurasa 43
Hatua 2: Soma kwa sauti	Ukurasa 43
Hatua 3: Jadili	Ukurasa 44
Hatua 4: Ongoza tendo	Ukurasa 45
Hatua 5: Simamia mazoezi	Ukurasa 46
Hatua 6: Jaza fomu ya kutathmini somo	Ukurasa 47
<b>Usuli wa somo kwa walimu</b>	Ukurasa 47

---

## Malengo ya Somo 4

Kile watoto wanafaa kujifunza katika somo hili:

- Kwanini hizi ni jinsi mbaya ya madai ya matibabu:
  1. Mwenye kuuza tiba kusema kitu juu yake
  2. Mtaalam amesema kitu juu ya tiba

---

## Matayarisho ya Somo 4(dakika 20)

Unachofaa kufanya kabla somo hilo.

### ***Soma mbele***

- Soma kurasa za somo hili katika vitabu vya watoto
- Soma kurasa za somo hili katika mwongozo

### ***Kusanya vifaa***

Hakikisha una:

- Mwongozo huu
- Fomu ya kutathmini somo hili
- Vifutio

### ***Hakikisha kuwa kila mtoto ana:***

- Nakala ya kitabu cha watoto
- Vitabu vyao vya mazoezi
- Penseli au kalamu

***Hadithi kwa ufupi:***Yohana na Julia wanakutana na Profesa Linganisha na Profesa Usawa sokoni. Yohana na Julia wamekusanya madai kutoka kwa watu huko sokoni. Hao Profesa wanachagua madai matatu ya kutumia kama mifano kueleza viini vingine viwili vya madai kuhusu matokeo ya matibabu. Kwanza, Profesa hao wanatumia madai ya Bw. Mwaka na Bi. Nantaba kama mifano. Dai la Bw. Mwaka ni kuhusu ndizi na la Bi. Nantaba Ni kuhusu maembe. Ya pili, hao Profesa wanatumia dai la Bi. Namuli kama mfano. Dai la Bi. Namuli ni kuhusu mashini ndogo ya stima.

## Somo 4(dakika 80)

This is a suggested plan for teaching the lesson.

Walimu	Watoto	Wakati
HATUA 1	Pitia somo lililopita	Dak 10-
<ul style="list-style-type: none"> <li>Pitia somo lililopita kwa kuuliza maswali ya ukurasa unaofuata.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali unavyoagizwa.</li> </ul>	
HATUA 2	Soma kwa sauti	Dak 25
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza kusoma kwa sauti kutoka kitabu cha watoto. <i>Kwa njia tofauti za kusoma kwa sauti aangalia ukurasa katika mwongozo huu</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa62 katika vitabu vyao na kusoma kwa sauti kulingana na maagizo.</li> </ul>	
	Pumziko	Dak 5
HATUA 3	Jadili	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Jadili hadithi kwa kuuliza maswali yaliyomo ukurasa unaofuatia katika mwongozo huu.</li> <li>Ikibidi, peana mifano ya ziada inayopatikana katika kurasa zinazofuata katika mwongozo huu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 4	Ongoza tendo	Dak 15
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza tendo. Angalia kurasa zinazofuata katika mwongozo huu na ukurasa 73 wa kitabu cha watoto.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa73 katika vitabu vyao na kufanya matendo kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 5	Simamia mazoezi	Dak 10

<ul style="list-style-type: none"> <li>Simamia mazoezi. Wasaidie wanafunzi wanapomaliza mazoezi yao na uongoze kusahihisha mazoezi yao.</li> </ul> <p><i>Kwa njia tofauti za kusahihisha angalia ukurasa katika mwongozo huu.</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa 20 katika vitabu vyao vya mazoezi na maliza mazoezi.</li> </ul>	
<b>HATUA 6</b>	<b>Jaza fomu ya kutathmiini</b>	Dak 5
Jaza fomu ya kutathmini somo		

---

## HATUA 1 – Pitia somo lililopita

Haya ni maswali na majibu ya kuptitia somo lililopita, na watoto.

### 1. Dai la Ruth ni lipi?

- Dai la Ruthni kuwa mitishamba yake hutibu magonjwa.

### 2. Kwa nini dai la Ruthhalikuwa linaaminika?

- Kiini cha dai la Ruth ilikuwa kuwa watu wengi walishatumia mitishamba yenewe kwa muda mrefu.Idadi ya watu ambao washatumia matibabu au muda ambao watu wengi washaitumia ni misingi mibaya ya madai kuhusu matibabu. Kuna matibabu mengi ambayo yanetumiwa na watu wengi kwa muda mrefu yaliyo na matokeo mengine kuliko yanayofikiriwa na watu – kwa mfano, kupaka mavi ya ng'ombe palipoungua.

### 3. Dai la Ahmed lilikuwa nini?

- Dai la Ahmedlilikuwa kwamba miwani yake ilikuwa bora kuliko miwani zingine.

### 4. Kwa nini dai la Ahmed halikuaminika?

- Kiini cha dai la Ahmed kilikuwa kwamba miwani yake ilikuwa mpya nay a bei ghali kuliko miwani zingine.Upya wa matibabu au bei yake ni misingi mibaya ya madai kuhusu matokeo yya matibabu. Matibabu ya zamani yenze bei ndogo yanaweza kuwa nzuri au hata bora zaidi kuliko matibabu mpya. Ahmed alliona vizuri vile aliona na hizo mpya.

---

## HATUA 2 – Soma kwa sauti(kitabu cha watoto ukurasa 62)

Maandishi yanaanza ukurasa 62 katika kitabu cha watoto.

**Usuli wa ukurasa 67:** Ndizi zina virutubishi vya potasiamu na vinyuzi. Zote zinaweza kuwa bora kwa afya yako. Pia zina vitamini B6 na vitamini A ambayo mwili wako waihitaji. Maembe ina vinyuzi na vitamin A,C na vitamin zingine muhimu. Kwa hivyo twasema kuwa kula ndizi na maembe ni bora kwa maisha yako kwa njia tofauti.

**Usuliwaukurasa 69:** Usuli: Watafiti wa afya wamechunguza mashini kama hizi na kupata kuwa hawazuii mbu kumfikia mtu na, kwa hivyo,hazikukingi kupata malaria.

**Maelezoukuras 70:** Madai ya mabingwa yaaminika kama kiini chake ni ulinganishaji wa haki na watu wengi, vile watoto watajifunza katika upande unaofuata kwenye kitabu.

---

## HATUA 3 – Jadili

Haya ni maswali na majibu ya kupidia yale mlisoma kwa sauti, na watoto.

#### **1.Dai la Bw. Mwaka ni lipi?**

- Ndizi ni bora kwa afya yako kuliko maembe.

#### **2.Dai la Bi. Nantaba ni lipi?**

- Maembe ni bora kwa afya yako kuliko ndizi.

#### **3.Kwa nini madai ya Bw. Mwaka na Bi. Nantaba hayaaminiki?**

- Kiini cha madai yao ni wauzaji wa matunda yenye ndiyo wanasema kitu juu yao. Anayeuzza matibabu atapata pesa zaidi kama watu wakiamini kuwa matibabu yana matokeo mazuri. Hiyo ndiyo yaweza kuwa sababu yake kudai kuwa hayo matibabu yana matokeo mazuri, kama inafanya hivyo au la.

#### **4.Dai la Bi. Namuli ni lipi?**

- Bi. Namuli alidai kuwa mashini yake ndogo ya stima inawazuia watu kupata malaria.

#### **5.Kwa nini dai la Bi. Namuli haliaminiki?**

- Kiini cha dai la Bi. Namuli likuwa kilichosemwa na bingwa. Hiki ni kiini kibaya cha dai hilo. Kwa mfano, kama dai la bingwa kuhusu matokeo ina kiini cha tajriba yake mwenye akitumia matibabu, basi dai lake haliaminiki nan i kiini kibaya cha mtu mwengine kudai kuhusu matokeo yake.

### **Mifano ziada ya kuwapa watoto, ikibidi**

Hii ni mifano ya ziada ya kusaidia kueleza kile watoto wangejifunza kutoka kwenye hadithi. Tumia tu mifano hii ukiona inabidi.

*Kwa nini kile mtu anayeuzza matibabu anachokisema kukihusu ni kiini kibaya cha madai kuhusu matokeo ya matibabu.*

**Dai:** “Sabuni hii itafanya ngozi yako iwe laini zaidi! Aliyeniuzia aliniambia hivyo!”

**Matibabu:**Kutumia hiyo sabuni

**Matokeo:**Kuwa na ngozi laini zaidi

**Kiini:**Kile kilichosemwa kuhusu sabuni na aliyekuwa anauza

**Maelezo:**Kile kilichosemwa juu ya sabuni na aliyekuwa akiuza ni kiini kbaya cha dai. Inawezekana kuwa huyo mtu anasema ili atengeneze pesa zaidi. Dai hilo haliaminiki.

*Kwa nini kile bingwa anasema kuhusu matibabu ni kiini kibaya cha madai kuhusu matokeo ya matibabu.*

**Dai:** “Mtaalamu wa mitishamba aliniambia kuwa hii chai itanitibu misuli yangu inayouma. Lazima iwe ukweli kwani yeye ni mtaalamu wa chai! Alisema ana uhakika kwa sababu watu wameinywa hiyo chai kwa maumivu ya misuli kwa miaka mingi.”

**Matibabu:**Kunywa hiyo chai ya mitishamba

**Matokeo:**Kumaliza maumivu ya misuli

**Kiini:**Kilichosemwa na huyo mtaalamu

**Maelezo:**Kilichosemwa na mtaalamu ni kiini kibaya cha dai. Kiini chake kilikuwa muda ambao watu wametumia chai kwa maumivu ya misuli. Inawezekana kuwa hiyo chai haina matokeo yoyote kwa maumivu ya misuli. Pia inawezekana kuwa chai yenyewe ina matokeo mabaya. Dai haliaminiki.

---

## **HATUA 4 – Ongoza tendo (kitabu cha watoto ukurasa 73)**

Tendo linaanza ukurasa73wa kitabu cha watoto.

**Maagizo ya ziasa:**Andika viini ambavyo watoto wamejifunza ubaoni:

- Tajriba ya mtu mwenyewe akitumia matibabu
- Muda ambao matibabu yashatumiwa au idadi ya watu ambao washayatumia
- Bei ya matibabu au upya wa matibabu
- Kuwa anayeyauza matibabu anasema kitu kuihusu
- Kuwa bingwa wa hicho kitu anasema kitu kuhusu matibabu

**Hatua 5:**Ni muhimu kulihusisha darasa zima.

### **Orodha ya madai kwa tendo**

*Dai la Alexandra: "Kula nyama zaidi itakufanya uwe mwenye nguvu zaidi na mwerevu zaidi! Niliisikia kutoka kwa muuza nyama!"*

**Matibabu:**Kula nyama zaidi

**Matokeo:**Kuwa na nguvu zaidi na mwerevu zaidi

**Kiini:**Kile muuza nyama alimwambia Alexandra

**Maelezo:**Dai hili haliaminiki. Inawezekana kuwa muuza nyama anasema haya ili auze nyama nyingi zaidi na apate pesa zaidi.

*Dai la Kate: "Ukiwa na maumivu ya kichwa, unafaa kuweka taweli katika maji baridi, halafu iweke taweli kichwani mwako! Itapunguza maumivu! Watu wengi huyafanya haya!"*

**Matibabu:**Kuweka taweli kwenye maji baridi halafu kichwani mwako

**Matokeo:**Kutuliza maumivu ya kichwa

**Kiini:**Idadi ya watu ambao wametumia matibabu

**Maelezo:**Dai haliaminiki. Inawezekana kuwa kuweka taweli ndani ya maji baridi kasha kichwani mwako hakuna matokeo yoyote kwa maumivu yako ya kichwa.

*Dai la Patrick: "Kula chokoleti inaponyesha maumivu ya kichwa! Najua kwa sababu nilijaribu kula chokoleti nilipokuwa naumwa na kichwa na maumivu yakapotea haraka sana!"*

**Matibabu:**Kula chokoleti

**Matibabu:**Kumaliza maumivu ya kichwa

**Kiini:**Tajriba ya Patrick ya kula chokoleti

**Maelezo:**Dai haliaminiki. Inawezakuwa maumivu ya kichwa ya Patrick yangeisha haraka hata kama asingekula chokoleti.

*Dai la Agnes: "Kutafuna majani ya chai kunamaliza maumivu ya tumbo! Mtaalamu wa mitishamba aliniambia na yeye ni mtaalamu wa matibabu ya aina hii! Mtaalamu alisema kuwa kwamuda mrefu, watu wametafuna majani ya chai kwa maumivu ya tumbo!"*

**Matibabu:**Kutafuna majani ya chai

**Matibabu:**Kupunguza maumivu ya tumbo

**Kiini:**Kilichosemwa na mtaalamu wa mitishamba kuhusu kutafuna majani ya chai

**Maelezo:**Dai haliaminiki. Dai la mtalaamu inaegemea muda ambao watu wametafuna majani ya chai kwa maumivu ya tumbo. Inawezekana kuwa kutafuna majani ya chai hakuleti matokeo yoyote hata ikiwa watu washafanya hivyo kwa muda mrefu.

*Dai la Ali: "Haya maziwa yatakufanya uwe na nguvu zaidi kuliko maziwa mengine! Na ni ya bei ghali!"*

**Matibabu:** Kunywahiyomaziwa

**Matokeo:**Kuwa na nguvu zaidi

**Kiini:**Bei ya maziwa

**Maelezo:**Dai hili haliaminiki. Inawezekana kuwa kunywa maziwa mengine kunaweza kukufanya uwe na nguvu au hata zaidi.

---

## HATUA 5 – Simamia mazoezi(kitabu cha mazoezi ukurasa 20)

Watoto wanatarajiwa kuandika majibu katika vitabu vyao vyta mazoezi.

**Maagizo ziada:**Wakumbushe watoto wakusanye madai nyuma ya vitabu vyta mazoezi.

### Majibu ya mazoezi ya Somo la 4:

#### ZOEZI 1

1. **Kweli** Uongo
2. **Kweli** Uongo
3. **Kweli** Uongo
4. **Kweli** Uongo

#### ZOEZI 2

1. *Dai haliaminiki kwa sababu:*Kiini ni kwamba wanaouza matibabu walisema kitu yake. Hiki ni kiini kibaya cha dai hili.
2. *Dai haliaminiki kwa sababu:*Kiini ni kuwa mtaalamu alisema kitu kuhusu matibabu hayo. Hiki ni kiini kibaya cha dai.

---

## **HATUA 6 – Jaza fomu ya kutathmini somo**

---

### **Usuli wa Somo 4 kwa walimu**

Watu wanaouza matibabu hutoa madai mengi kuhusu matokeo. Ni lazima kila mara ujilize kama kiini cha madai hayo ni mazuri au mabaya. Ni rahisi kupotoshwa kwa sababu unafikiri kuwa kama matibabu inauzwa na watu wengi wanailipia, lazima ilifanyia kipimo toshelezi. Madai kuhusu matibabu kama haya yanaweza kuonekana kama maelezo ya kinachotolewa dai, na kumbe ni madai tu kama mengine.

Watu wanaouza matibabu wana sababu kadha. Sababu ina maana ya kitu kitakachowafaidi. Wana upendeleo kwa matibabu wanayouza kuwasaidia wateja wao. Hata hivyo, wana sababu ya kujichumia pesa. Hizi sababu mbili zinashindana. Inaitwa mgongano wa sababu. Saa zingine, wakati mwuzaji ana mgongano wa sababu, wao hutoa madai yasiyoaminika kuhusu matokeo kwa sababu ya mgongano.

Wataalamu pia saa zingine hutoa madai yasiyoaminika. Kwa mfano, madaktari na wataalamu wengine wamesema kuwa kupumzika kitandani kwa muda mrefu inafaa kwa magonjwa mengi tofauti, kama afkani na maumivu ya mgongo. Wataalamu wengine hawakubaliani. Watafiti wa afya walipata kuwa matokeo mazuri ya matibabu haya si mazuri vile. Walipata kuwa haya matibabu hayakuwa na matokeo mazuri hata kidogo kwa kwa kesi zingine. Kuongezea, walipata kuwa kupumzika kwa muda mrefu unaezza kuwa na matokeo mabaya. Mara nyingi, wataalamu hawakubaliani kuhusu matokeo ya matibabu. Wote ni wataalamu, lakini si wote wanaweza kuwa sawa.

## SOMO 5

### Kulinganisha matibabu

Kila kitu unachohitaji kutayarisha na kufunza hili somo:

<b>Malengo</b>	Ukurasa 49
<b>Matayarisho</b>	Ukurasa 49
<b>Somo:</b>	
Hatua 1: Pitia somo lililopita	Ukurasa 52
Hatua 2: Soma kwa sauti	Ukurasa 52
Hatua 3: Jadili	Ukurasa 52
Hatua 4: Ongoza tendo	Ukurasa 53
Hatua 5: Simamia mazoezi	Ukurasa 53
Hatua 6: Jaza fomu ya kutathmini somo	Ukurasa 54
<b>Usuli wa somo kwa walimu</b>	Ukurasa 54

---

## Malengo ya Somo 5

Kile watoto wanafaa kujifunza katika somo hili:

- Chanzo cha lazima kwa wataalamu wa afya kulinganisha tiba moja na nyingine au kukosa tiba.

## Matayarisho ya Somo(dakika 20)

Unachofaa kufanya kabla somo hilo.

### ***Soma mbele***

- Soma kurasa za somo hili katika vitabu vya watoto
- Soma kurasa za somo hili katika mwongozo

### ***Kusanya vifaa***

Hakikisha una:

- Mwongozo huu
- Fomu ya kutathmini somo hili
- Vifutio

### ***Hakikisha kuwa kila mtoto ana:***

- Nakala ya kitabu cha watoto
- Vitabu vyao vya mazoezi
- Penseli au kalamu

***Hadithi kwa ufupi:***Yohana na Julia wanaizuru ofisi ya hao Profesa katika chuo kikuu. Hao Profesa wanaanza kuwafunza Yohana naJulia kuhusu madai ya kuaminika, yanayotegemea utafiti wa afya. Hao Profesa wakaanza kuwaeleza kile utafiti wa afya lazima ufanye ili kupata mengi kuhusu matokeo ya matibabu. Kwanza, lazima waligeuze dai lolote kuhusu matibabu liwe swalii. Ya pili, lazima walinganishe matibabu kwa matibabu mengine au na bila matibabu.Hiyo inamaanisha lazima wapeane matibabu moja kwa kikundi kimoja cha watu na matibabu tofauti au kutopeaana matibabu yoyote kwa kikundi tofauti cha watu. Ya tatu, lazima wapime kilichofanyika na kulinganisha kilichofanyika katika hivyo vikundi tofauti.

## Somo 5(dakika 80)

This is a suggested plan for teaching the lesson.

Walimu	Watoto	Wakati
HATUA 1	Pitia somo lililopita	Dak 10-
<ul style="list-style-type: none"> <li>Pitia somo lililopita kwa kuuliza maswali ya ukurasa ufuatao.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 2	Soma kwa sauti	Dak 25
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza kusoma kwa sauti kutoka kitabu cha watoto. <i>Kwa njia tofauti za kusoma kwa sauti aangalia ukurasa katika mwongozo huu</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 80 katika vitabu vyao na kusoma kwa sauti kulingana na maagizo.</li> </ul>	
	Pumziko	Dak 5
HATUA 3	Jadili	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Jadili hadithi kwa kuuliza maswali yaliyomo ukurasa unaofuatia katika mwongozo huu.</li> <li>Ikibidi, peana mifano ya ziada inayopatikana katika kurasa zinazofuata katika mwongozo huu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 4	Ongoza tendo	Dak 15
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza tendo. Angalia kurasa zinazofuata katika mwongozo huu na ukurasa 93 wa kitabu cha watoto.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 93 katika vitabu vyao na kufanya matendo kulingana na maagizo.</li> </ul>	
HATUA 5	Simamia mazoezi	Dak 10

<ul style="list-style-type: none"> <li>Simamia mazoezi. Wasaidie wanafunzi wanapomaliza mazoezi yao na uongoze kusahihisha mazoezi yao.</li> </ul> <p><i>Kwa njia tofauti za kusahihisha angalia ukurasa katika mwongozo huu.</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa 26 katika vitabu vyao vya mazoezi na maliza mazoezi.</li> </ul>	
<b>HATUA 6</b>	<b>Jaza fomu ya kutathmiini</b>	Dak 5
Jaza fomu ya kutathmini somo		

---

## HATUA 1 – Pitia somo lililopita

Haya ni maswali na majibu ya somo lililopita, na watoto.

### 1. Dai la Bw. Mwaka lilikuwa lipi?

- Kuwa ndizi ni bora kwa afya yako kuliko maembe.

### 2. Dai la Bi. Nantaba ni lipi?

- Kuwa maembe ni bora kwa afya yako kuliko ndizi.

### 3. Kwa nini madai Bw. Mwaka na Bi. Nantaba hayaaminiki?

- Kiini cha madai kilikuwa watu wanaouza matunda kusema kitu juu yake. Anayeuzza matibabu atapata pesa nyingi zaidi watu wakiamini kuwa matokeo yana matokeo mazuri. Hii inaweza kuwa sababu ya kuwa huyo mtu anadai kuwa matibabu hayo yana matokeo mazuri, ikiwa ni kweli au la.

### 4. Dai la Bi. Namuli lilikuwa lipi?

- Bi. Namuli alidai kuwa mashini yake ndogo ya stima yawazuia watu kupata maleria.

### 5. Kwa nini dai la Bi. Namuli halikuaminika?

- Kiini cha dai la Bi. Namuli kilikuwa kile mtaalamu alisema. Hiki ni kiini kibaya cha dai. Kwa mfano, kama dai la mtaalamu kuhusu matokeo inaegemea tajriba ya mtu binafsi kutumia matibabu, dai la mtaalamu huyo haliaminiki na ni kiini kibaya cha dai la mtu mwengine kuhusu matokeo.

---

## HATUA 2 – Soma kwa sauti (kitabu cha watoto ukurasa 80)

Maandishi yanaanza ukurasa 80 katika kitabu cha watoto.

**Usuli wa ukurasa 92:** Usuli: Watafiti wamelinganisha watu wanaolalachini ya neti zilizonyunyiziwa dawa ya kuua wadudu kwa watu ambao hawalali chini ya neti au wanaolala chini ya neti zisizonyunyiziwa dawa. Neti zilizonyunyiziwa dawa ya kuua wadudu zina uwezo mkuu wa kupunguza idadi ya watoto wanaopata malaria na kufa kutokana na malaria.

---

## HATUA 3 – Jadili

Haya ni maswali na majibu za kufanya marudio ya uliyosoma kwa sauti, pamoja na watoto.

### 1. Ni hatua gani ya kwanza ambayo watafiti wa afya huchukua ili kuchunguza zaidi kuhusu matokeo ya matibabu?

- Hugeuza dai kuwa swali la utahini.

## **2. Ni matibabu gani ambayo watafiti wa afya wanalinganisha kwa kutumia mashini ya Bi. Namuli?**

- Kutumia mashini kama stima imezimwa, ambayo ni sawa na kutotumia mashini.

## **3. Watafiti wa afya walipataje?**

- Walipata kuwa mashini yenyewe haikuwa na matokeo muhimu.

## **4. Watafiti wa afya walipataje kuhusu matokeo ya kulala chini ya neti za mbu?**

- Walipata kuwa iliwazuia watu kupata malaria kama neti zilinyunyiziwa dawa za kuua wadudu.

---

## **HATUA 4 – Ongoza tendo(kitabu cha watoto ukurasa 93)**

Tendo linaanza ukurasa wa 93 katika kitabu cha watoto.

### ***Tendo Sehemu 1***

**Hatua 2:** Sema, "Nyanya," au, "Viasi." Andika "Nyanya" na "Viasi" kwenye sehemu tofauti za ubao.

**Maelezo hatua 11:** Bila kulinganisha matibabu (kuweka mikono yako nyuma ya masikio yako) kwa matibabu mengine, huwezi kupata mengi kuhusu matokeo. Kwa mfano, inawezekana kuwa watoto zaidi wangesikia neno hilo kama wasingeweka mikono yao nyuma ya masikio yao.

### ***Tendo Sehemu 2:***

**Hatua:** Watoto wabaki katika madawati yao. Gawa darasa kwa vikundi viwili kati ya walio mbele na walio nyuma ya darasa. Waliopo mbele ya darasa ni Kikundi 1.

**Hatua 3:** Sema "Kuomba," au, "Kuimba." Andika "Kuimba" na "Kuomba" katika sehemu mbili za ubao.

**Maelezohatua 14:** Maelezo: Baada ya kulinganisha, ulipata kuwa matibabu (kuweka mikono yako nyuma ya masikio yako) inakusaidia kusikia vizuri zaidi, haileti tofauti yoyote au inakuzuia kusikia vizuri. Hata hivyo, huwezi kuwa na uhakika kuwa uliyopata ndiyo matokeo ya matibabu kwa vile ulinganisho haukuwa wa haki na ulikuwa mdogo sana. Watoto wastajifunza zaidi kuhusu haya katika masomo mawili yanayofuatia.

---

## **HATUA 5 – Simamia mazoezi(kitabu cha mazoezi ukurasa 26)**

Watoto wanafaa kuandika majibu katika vitabu vyao vya mazoezi.

**Maagizo ya ziada:** Wakumbushe watoto wakusanye madai nyuma ya vitabu vyao. Vya mazoezi.

## Majibu ya mazoezi ya Somo 5:

### ZOEZI 1

1. Dai la kuaminika ni dai lenye kiini kizuri.
2. Kulinganisha matibabuni kuangalia tofauti kati ya matibabu mawili au zaidi.
3. Kupima ni kuangalia kitu kinatoshaje au ni cha idadi gani.

### ZOEZI2

- |                                    |           |
|------------------------------------|-----------|
| 1. <b><u>Wapime kwa saa</u></b>    | Waulize   |
| 2. <b><u>Shika vichwa vyao</u></b> | Wanuse    |
| 3. <b><u>Waulize</u></b>           | Waangalie |

### ZOEZI3

*Watu wangapi walikuwa na maleria katika kila kikundi?*

Kikundi A: **5**kati ya 20

Kikundi B: **11**kati ya 20

*Tofaut gani ilikuwa kati ya vikundi?*

Kulikuwa na watu**6**walio na malaria kati ya watu 20 katika Kikundi **B**.

---

*Watu wangapi walikuwa na malaria katika kila kikundi?*

Kikundi A: **17**kati ya 50

Kikundi B: **25**kati ya 50

*Tofauti gani ilikuwa kati ya vikundi?*

Kulukuwa na watu**8**zaidi waliokuwa na malaria kati ya watu 50 katika Kikundi **B**.

---

## HATUA 6 – Jaza fomu ya kutathmini somo

---

### Usuli wa Somo la 5 kwa walimu

Haiwezekani kujua matokeo ya matibabu bila kuilinganisha na kitu chengine. Mara nyingi, watafiti wa afya hulinganisha kinachotendeka kwa kikundi kimoja cha watu wanaotumia matibabu hayo kwa kikundi chengine cha watu ambao hawakutumia matibabu hayo. Mara nyingine, walio kwenye kikundi chengine hupewa matibabu tofauti.

Kwa mfano, kabla watafiti wa afya kulinganisha kutumia mitishamba inayoitwa valerian na kutoitumia, haikuwezekana kamwe kuwa na uhakika matokeo yake. Watu wengine waliamini kuwa valerian ingesaidia kulala vizuri kama ulikuwa na shida ya kulala. Dai hili lilitokana na tajriba ya watu binafsi. Mwishowe, watafiti wa afya walilinganisha kutumia valerian na kutumia matibabu yaliyofanana na kuwa na harufu sawa na valerian, lakini hayakuwa na viungo vitumikavyo. Matibabu bandia kama haya yanaitwa

'placebo'. Walipeana valerian kwa kikundi kimoja cha watu na kupeana placebo kwa kikundi chengine. Kisha wakalinganisha kilichotendeka katika kila kikundi wakapata kuwa hakukuwa na tofauti kubwa au hakukuwa na tofauti yoyote. Walipata kuwa valerian haikuwa na matokeo yoyote au matokeo madogo katika vile mtu alilala ikilinganishwa na matokeo ya placebo.

Kabla watafiti wa afya hawajalinganisha, lazima wawe na swali la kitafiti. Hutengeneza maswali ya kitafiti kwa kugeuza madai kuwa maswali. Kwa mfano, waligeuza dai kuwa valerian inakusaidia kulala vizuri zaidi kuwa swali kuhusu kama inafanya hivyo. Sayansi na utafiti, zote huanza na kuuliza kama kinachoaminiwa na watu ni sawa, hata kama kile kinachoaminiwa na wanasayansi na watafiti. Hatua inayofuatia ni kuchunguza kwa makini ili kutafuta mengine zaidi, ili tuwe na uhakika zaidi kama hiyo imani ni sawa au uongo.

## SOMO 6

### Kulinganisha haki ya matibabu

Kila kitu unachohitaji kutayarisha na kufunza hili somo:

<b>Malengo</b>	Ukurasa 57
<b>Matayarisho</b>	Ukurasa 57
<b>Somo:</b>	
Hatua 1: Pitia somo lililopita	Ukurasa 60
Hatua 2: Soma kwa sauti	Ukurasa 60
Hatua 3: Jadili	Ukurasa 61
Hatua 4: Ongoza tendo	Ukurasa 62
Hatua 5: Simamia mazoezi	Ukurasa 63
Hatua 6: Jaza fomu ya kutathmini somo	Ukurasa 63
<b>Usuli wa somo kwa walimu</b>	Ukurasa 63

---

## Malengo ya Somo 6

Kile watoto wanafaa kujifunza katika somo hili:

- Kufafanua maana ya kulinganisha matibabu kwa hali
  - Sababu ya watafiti wa kiafya kuhitajika kuwa na haki wakilinganisha matibabu tofauti
  - Jinsi watafiti wa kiafya wanapaswa kuwa na haki wakilinganisha matibabu tofauti
- 

## Matayarishoya Somo 6(dakika 20)

Unachofaa kufanya kabla somo hilo.

### ***Soma mbele***

- Soma kurasa za somo hili katika vitabu vya watoto
- Soma kurasa za somo hili katika mwongozo

### ***Kusanya vifaa***

Hakikisha una:

- Mwongozo huu
- Fomu ya kutathmini somo hili
- Vifutio

### ***Hakikisha kuwa kila mtoto ana:***

- Nakala ya kitabu cha watoto
- Vitabu vyao vya mazoezi
- Penseli au kalamu

***Hadithi kwa ufupi:*** Hao Profesa wanawapata Yohana na Julia uwanjani katika kijiji chao. Yohana na Julia wamewakusanya marafiki 10. Hao wanawafunza Yohana na Julia zaidi kuhusu utafuti wa afya. Wanalinganisha pamoja, ili Yohana na Julia wajifunze kwa nini na vile watafiti wa afya lazima wawe na haki wanapolinganisha matibabu. Swali lao la utafuti ni: Kama kunywa sharubeti kabla ya kukimbia huwapa watu wengi zaidi maumivu ya tumbo ikilinganishwa na kunywa maji?

## Somo 6(dakika 80)

Huu ni mpango uliopendekenzwa wa kufunzia somo hili.

Walimu	Watoto	Wakati
<b>HATUA 1</b>	<b>Pitia somo lililopita</b>	Dak 10-
<ul style="list-style-type: none"> <li>Pitia somo lililopita kwa kuuliza maswali katika ukurasa ufuatao.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 2</b>	<b>Soma kwa sauti</b>	Dak 25
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza kusoma kwa sauti kutoka kitabu cha watoto. <i>Kwa njia tofauti za kusoma kwa sauti aangalia ukurasa katika mwongozo huu</i></li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 100 katika vitabu vyao na kusoma kwa sauti kulingana na maagizo.</li> </ul>	
	<b>Pumziko</b>	Dak 5
<b>HATUA 3</b>	<b>Jadili</b>	Dak 10
<ul style="list-style-type: none"> <li>Jadili hadithi kwa kuuliza maswali yaliyomo ukurasa unaofuatia katika mwongozo huu.</li> <li>Ikibidi, peana mifano ya ziada inayopatikana katika kurasa zinazofuata katika mwongozo huu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jibu maswali kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 4</b>	<b>Ongoza tendo</b>	Dak 15
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ongoza tendo. Angalia kurasa zinazofuata katika mwongozo huu na ukurasa 119 wa kitabu cha watoto.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa wa 119 katika vitabu vyao na kufanya matendo kulingana na maagizo.</li> </ul>	
<b>HATUA 5</b>	<b>Simamia mazoezi</b>	Dak 10

<ul style="list-style-type: none"> <li>Simamia mazoezi. Wasaidie wanafunzi wanapomaliza mazoezi yao na uongoze kusahihisha mazoezi yao.</li> </ul> <p><i>Kwa njia tofauti za kusahihisha angalia ukurasa katika mwongozo huu.</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Fungua ukurasa 32 katika vitabu vyao vya mazoezi na maliza mazoezi.</li> </ul>	
<b>HATUA 6</b>	<b>Jaza fomu ya kutathmiini</b>	Dak 5
Jaza fomu ya kutathmini somo		

---

## HATUA 1 – Pitia somo lililopita

Haya ni maswali na majibu ya kupertia somo lililopita, na watoto.

### 1. Hatua ya kwanza ambayo watafiti wa afya huchukua kutafuta zaidi kuhusu matokeo ya matibabu ni nini?

- Wanageuza dai kuwa swali la utafiti.

### 2. Ni matibabu gani ambayo watafiti wa afya wanalinganisha na kutumia mashini ya Bi. Namuli?

- Kutumia mashini ikiwa imezimwa, ambayo ni sawa na kutotumia mashini.

### 3. Watafiti wa afya walipataje?

- Walipata kuwa hiyo mashini haikuwa na matokeo yoyote ya muhimu.

### 4. Wafiti wa afya walipataje kuhusu matokeo ya kulala ndani ya neti ya kuzuia mbu?

- Walipata kuwa ilizuia watu kupata malaria kama neti zilinyunyiziwa na kiuwa wadudu.

---

## HATUA 2 – Soma kwa sauti (kitabu cha watoto ukurasa 100)

Maandishi yanaanza ukurasa 100 katika kitabu cha watoto.

**Maelezo ukurasa 106:** Baadaye katika hadithi, hao Profesa wanatumia kile Yohana, Julia na marafiki zao wanajibu ili kueleza tatizo ambalo linaweza kufanya ulinganisho unaweza kutokuwa wa haki. Hili swali la kujadiliwa liko hapa ili watoto wa darasa wakumbuke kile Yohana, Julia na marafiki zao walijibu. **Maagizo:** waambie watoto darasani mwako wajibu maswali ya Profesa Linganisha.

**Maelezo ukurasa 107:** Katika utafiti wa afya, “kutokuwa na haki” ni pale kuna tofauti muhimu kati ya vikundi vyta watu wanaoltinganishwa au vile wanavyotendewa, vile wanapata matibabu yao ama vile kinachowafanyikia kinapimwa.

**Maelezo ukurasa 110:** Katika somo lijalo, watoto watajifunza kuhusu kupata kitu kibahati katika ulinganisho ulio mdogo sana. “Kibahati” haina maana sawa ukizungumzia kuhusu kuchagua kitu kama wakati unazungumzia kupata kitu.

---

## HATUA 3 – Jadili

Haya ni maswali na majibu ya kurudia ulichosoma kwa sauti, na watoto.

### 1. Ulinganisho wa haki wa matibabu ni nini?

- Ni ulinganisho ambao tofauti yake muhimu pekee kati ya vikundi ni matibabu yanayoltinganishwa.

### 2. Ni tatizo gani linaweza kufanya ulinganisho uwe usio na haki?

- Watu kuchagua nani anapewa matibabu gani.

### 3. Yohana, Julia na hao Profesa walitatuaje tatizo la kwanza?

- Walirusha senti juu kuchagua nani angepewa sharubati na nani angepewa maji. Kwa kufanya hivi, vikundi vilifanana zaidi kwa vile kila mmoja wao walikuwa na nafasi sawa ya kupata sharubeti.

### 4. Ni tatizo gani la pili linaloweza kufanya ulinganisho usiwe wa haki?

- Watu wakijua matibabu waliyopata.

### 5. Yohana, Julia na hao Profesa walitatuaje tatizo la pili?

- Profesa Linganisha alichanganya poda kwa maji ikafanya hicho kinywaji kuonekana na kuwa na ladha ya sharubeti. Hivi, marafiki walioinywa hawakuja kama wanakunyuwa sharubati yenye. Kumbuka kuwa, watoto wote walidhani kuwa kunyuwa sharubeti kabla kukimbia huwapa watu wengi maumivu ya tumbo ikilinganishwa na kunyuwa maji. Kwa hivyo, wangejua aliyepata nini, wale walikunyuwa sharubeti wangefikiria kuwa wangepata maumivu ya tumbo zaidi. Kuna uwezekano wa wengine kusema walipata maumivu ya tumbo kwa sababu walifikiria wangepata.

## Mifano ziada kuwapatia watoto, ikibidi

Hii ni mifano ya ziada ya kusaidia kueleza kile ambacho watoto wangejifunza kutoka kwa hadithi hiyo. Tumia tu mifani hii ukidhani inabidi.

*Kwa nini mtu anayechagua watu wanaoenda kwa vikundi tofautii inaweza kufanya ulinganisho usiwe wa haki*

**Swali la utafiti:** Kucheza densi angaa mara moja kwa wiki huwafanya watu kuwa na furaha ikilinganishwa na kutocheza densi kabisa?

**Vile watafiti walitengeneza vikundi:** Wanawawacha watu wachague kama wanataka kucheza densi. Watu wenye furaha zaidi walichagua kucheza densi.

**Maelezo:** Kuna tofauti muhimu kati ya vikundi kwa sababu watu wenye walechagua matibabu yao. Watu wenye furaha sana walikuwa katika kikundi kimoja. Kama watafiti wa afya wamepata kuwa waliochza densi wana furaha zaidi, inaweza kuwa walikuwa wenye furaha kutoka mwanzoni, si kwa sababu ya kucheza densi.

*Vile kutengeneza vikundi bila yeyote kuchagua anayeingia kikundi kipi*

**Mfano 1:**Changanya kadi za karatasi manjano na kijani kibichi. Kila mtu achukue kadi moja bila kuiangalia.Wakipata kadi ya kijani kibichi, wanaenda katika kikundi cha kwanza.Wakipata kadi ya manjano, wanaenda katika kikundi cha pili.

**Mfano 2:**Wape watu dadu. Kila mtu azungushe moja. Ikionyesha 1, 2 au 3, huyo mtu anaingia kikundi cha kwanza. Ikionyesha 4, 5 au 6, huyo mtu anaingia kikundi cha pili.

*Kwa nini mtu akijua aliyepata matibabu gani inaweza kufanya ulinganisho usiwe wa haki*

**Swali la utafiti:**Ni kweli kuwa, kuchukua tembe ya kumeza mpya inayogharimu bei zaidi hupunguza maumivu ya kichwa haraka zaidi kuliko tembe ya zamani?

**Vile watafiti waliunda vikundi:**Wanawapatia watu makasha ya tembe. Kwenye kasha, inaonyesha kama ina tembe mpya au ya zamani.

**Maelezo:**Kama watu wanafikiria tembe moja ni nzuri kuliko nyingine, kunakuwa na tofauti muhimu kati ya vikundi vyenyewe. Kwa mfano, kama watu weanafikiria kwamba hizo tembe mpya ni bora, basi watu kwenye kikundi wanaopata tembe mpya watakuwa na matumaini tofauti kuliko walio kwenye kikundi cha pili. Wanadhani maumivu yao ya kichwa yataisha haraka zaidi, kwa hivyo wanaweza kuhisi kuwa inapona haraka.

---

## **HATUA 4 – Ongoza tendo(kitabu cha watoto ukurasa 119)**

Tendo linaanza ukurasa 119 katika kitau cha watoto.

**Maelezo Hatua 1:** Katika somo lililopita, ulipogawa darasa mara mbili kati ya walio mbele ya darasa na walio nyuma. Watoto wote wa Kikundi 1 walikuwa mbele ya darasa. Watoto wote wa Kikundi 2 walikuwa nyuma ya darasa. Hiyo ilikuwa tofauti muhimu kati ya vikundi. Ulichopata katika tendo la Somo la 5, ingekuwa kwa sababu ya tofauti hii, si kwa sababu ya matibabu.

**Maelezo Hatua 2:**Kwa madarasa makubwa, mweke kila wa kwanza katika Kikundi 1, wa pili Kikundi 2, anayefuatia 1, anayemfuata 2 na kuendelea hivyo hadi waishe. Katika madarasa madogo, tumia senti kuchagua atakayekuwa kikundi kipi.

**Maelezo Hatua 3:**Sema mojawapo "Kuona," au, "Kupona." Andika "Kuona" na "Kupona" katika pande mbili tofauti ubaoni.

**Maelezo Hatua 14:** Ni vigumu kwa watoto kutojua aliyepata matibabu tofauti. Hii yaweza kuleta tofauti muhimu kati ya vikundi. Kama watoto wanafikiria kuwa kuweka mikono nyuma ya sikio kunakusaidia kusikia vizuri, kuna uwezekano kuwa watoto wa Kikundi 2 hawawezi kujaribu kusikia usemacho kwa kuwa watafikiria kuwa wasingesikia vizuri kama wa Kikundi 1.Watafiti wa afya lazima wazingatie umuhimu wa haya, wakilinganisha matibabu.

---

## **HATUA 5 – Simamia mazoezi (kitabu cha maoezi ukurasa 32)**

Watoto waandike majibu katika vitabu vyao vya mazoezi.

**Maagizoziada:** Wakumbushe watoto kukusanya madai nyuma ya vitabu vyao.

### **Majibu ya mazoezi ya Somo la 6:**

#### **ZEOZI 1**

1. **Kweli** Uongo
2. **Kweli** Uongo
3. **Kweli** Uongo
4. **Kweli** Uongo

#### **ZOEZI2**

1. Kwani kutumia dawa ya chanjo ya ukambi inawazuia watu kupata ukambi ukilinganisha na kutotumia dawa ya chanjo?
2. Hapana. Inaweza kufanya ulinganisho usiwe wa haki.
3. Hapana. Inaweza kufanya ulinganisho usiwe wa haki.
4. Hapana. Inaweza kufanya ulinganisho usiwe wa haki.

**Usuli wa Zoezi 2:** Watafiti wa afya wamechunguza dawa ya chanjo ya ukambi na wakapata kuwa inawazuia watu kupata ukambi bila kuwa ma matokeo mabaya mazito.

---

## **HATUA 6 – Jaza fomu ya kutathmini somo**

### **Usuli wa Somo 6 ya walimu**

Kunapokuwa na tofauti muhimu kati ya vikundi kwenye ulinganisho, mbali na matibabu, ulinganisho si wa haki. Wakati ambapo ulinganisho huo sio wa haki, kile watafiti wa afya wanapata unaweza kuwa kwa sababu ya hizo tofauti muhimu, na si kwa sababu ya matibabu yanayolinganishwa. Yamaanisha, hatuwezi kuwa na uhakika kuwa kilichotendeka kilikuwa matokeo ya matibabu. Matokeo kutokana kwa ulinganisho usio wa haki waweza kupotosha tusipofahamu kuwa ulinganisho haukuwa wa haki. Katika utafitiwa afya, makosa yanayofanya ulinganisho usiwe wa haki yanaitwa “makosa ya utaratibu” au “mapendeleo”. Katika somo hili, watoto wanajifunza aina mbili za makosa ya utaratibu.

Aina ya kwanza ni watu wanapokubaliwa kuchagua anayepewa matibabu gani. Kwa mfano, madaktari walidai kuwa wanawake wakitumia aina ya dawa iitwayo hormones, wachache wao watapata mshtuko wa moyo ama afkani. Kiini chengine cha dai kilikuwa ulinganisho usio wa haki. Ulinganisho ulikuwa kati ya vikundi vya wanawake waliomeza hormones na vikundi vya wanawake wasiochukua. Hao wanawake

walikubaliwa kuchagua kama wangemeza hormones. Wanawake wengine walikuwa wamejitunza kiafya kabla ulinganisho. Wengi wa wanawake kama hao walichagua kumeza hormones. Hii inamaanisha kuwa wanawake waliochagua kumeza hormones walikuwa wa hatari ya chini ya kupata afkani.

Hii ilikuwa tofauti muhimu kati ya vikundi vyenyewe. Mwishowe, watafiti wa afya walifanya malinganisho mapya pale walipochagua kibahati wanawake ambao walimeza hormones. Katika malinganisho haya ya haki, watafiti wa afya walipata kuwa wengi wa wanawake waliomeza hormones walipata afkani ukilinganisha na wale hawakumeza! Katika utafiti wa afya, kuchagua kibahati anayepewa matibabu gani inaitwa “gawia bila mpango”. Mara nyingi, watafiti wa afya hutumia mpango wa kompyuta ili “kugawia bila mpango” kila mtu kwa matibabu. Kugawa bila mpango haiwezekani kila mara na pia haina maadili. Kama kugawa bila mpango hakuwezekani, watafiti wa afya lazima wazingatie tofauti zingine muhimu kati ya vikundi.

Aina ya pili ya makosa ya utaratibu ambayo watoto watajifunza ni wakati watu wakikubaliwa kujua aliyepeata matibabu gani. Kwa mfano, kuna sehemu ya goti inayoitwa meniscus. Meniscus iliyochanuka ni madhara ya kawaida. Madaktari wapasuaji wamedai kuwa kuna upasuaji unaotibu madhara yenye na kupunguz maumivu. Kiini cha dai lao ilikuwa ulinganisho wa pale watu walijua kama walifanyiwa upasuaji huo. Mwishowe, watafiti wa afya walilinganisha kufanyiwa upasuaji na upasuaji bandia. Matibabu bandia inatwa “placebo”. Watafiti wa afya saa zingine hutumia placebos ili mtu asijue ni nani alipata nini. Hii huitwa “kupofusha”. Kwa upasuaji bandia, madaktari watakata pahali padogo katika goti la mgonjwa na kujifanya walifanya upasuaji. Watafiti walipata kuwa kikundi kilichofanyiwa upasuaji bandia, kuna wengi ambao walidai kuwa na uchungu uliopungua kama waliofanyiwa upassuaji wenyewe! Hata upofushaji pia hauwezekani kila mara.

## SOMO 7

